# MPENDWA ABDALLAH

## Barua kutoka kwa Theophilo

Huku ni kubadilishana barua za kufikiria zinazoelezea masuala yanayohusu Waislamu na Wakristo.

Jina “Abdallah” ni la Kiarabu na lina maana ya “Mtumishi wa Mungu”. Mwandishi anaitwa Theofilo; hili ni jina la Kibiblia kwa maana ya “Anayependwa na Mungu”.

Gerhard Nehls

Kichwa cha asili cha kitabu: Dear Abdallah

© 2022, kwa Toleo la Kiswahili
Life Challenge
P.O. Box 50770-00200,
Nairobi, KENYA
**www.life-challenge.org**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoruhusiwa kunakiliwa bila idhini ya maandishi, isipokuwa kwa nukuu fupi katika vitabu na mapitio.

Nukuu zote za Kurani zimetolewa kwenye: KURANI TAKATIFU, iliyofasiriwa na Sheikh Abdullah Saleh Farsi, chapa ya saba, 1993.

Nukuu za Biblia zimetolewa kwenye: NENO BIBLIA TAKATIFU, 2014.

Kimetafsiriwa na John Augustine Mabutagulwa, Zanzibar, Tanzania.

ISBN: 978-9966-895-66-0

Printed and bound in Kenya

04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 2 13-04-2022 12:22:08

# Mpendwa Abdallah

***Barua ya Kwanza***

## Wote tunakaa kwenye mashua moja

*Mpendwa Abdallah*

Ninaandika barua hii kukueleza furaha niliyo nayo kwa kukutana. Haitokei mara nyingi kwamba Mwislamu na Mkristo wanakutana kama tulivyofanya. Tuligundua mengi yanayofanana bila ya kujifanya kuwa hakupo kutofautiana. Sote tunazitambua tofauti kati ya imani zetu - na haja ya kuzifikiria. Ahadi yetu kuwa mazungumzo yetu yatafanyika kirafiki kulingana na mada, ninaliona kuwa ni jambo zuri sana. Yote ni kwa kumheshimu Mungu!

Ni vizuri kutambua kuwa sote tuna matumaini na matarajio yanayofanana sana kuhusu maisha. Lililonivutia hasa ni utambuzi wetu wa Mwenyezi Mungu. Wakati kuelewa kwetu kuhusu imani ya kidini huenda kukatofautiana, tunafanana sana katika hali ya undugu, upendo na uwezo wa kumhisi Mungu. Kwangu hili lina maana kuwa kimsingi wanadamu wana asili ya kumjua Mungu aliyoipanda ‘mioyoni’ mwetu.

Huenda linalohusiana na hilo, na ambalo ni muhimu sana kwangu, ni kuwa sote tuliitambua sana haja ya kuwa na moyo



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 1 13-04-2022 12:22:08

safi machoni kwa Mungu. Hili lina umuhimu wa kipekee maana Yesu aliwahi kusema kuwa ni wenye moyo safi tu watakaomwona Mungu (Mathayo 5:8).

Hili hunikumbusha Neno linalosema:

*Kama watoto watiifu, msifuate tamaa zenu mbaya wakati mlipoishi kwa ujinga. Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, nanyi kuweni watakatifu katika mwenendo wenu wote.* (1 Petro 1:14-15)

*Tafuteni ... utakatifu, ambao bila kuwa nao hakuna mtu atakayemwona Bwana.* (Waebrania 12:14)

Nina hakika sote tunautambua upungufu wetu wa usafi wa ndani. Mara nyingi mawazo na matendo yetu yote si matakatifu. Nadhani ndani ya mioyo yetu tunautambua upungufu wa kiroho unaosababishwa na dosari zetu, hata kama tunafuata sheria zetu za kidini. Kila makabiliano na kifo hutuletea maswali yanayosababisha tuhofie kifo – au hasa labda tuhofie kinachotokea baada ya kifo. Mtu anaweza kufurahia maisha mazuri kwenye mazingira ya kutokumjua Mungu, lakini hatimaye uhakika wa kufa huyaharibu yote, maana wote tunatambua kuwa, kama Biblia inavyoliweka:

"... sote tuna matumaini na matarajio yanayofanana sana kuhusu maisha."

*Kama vile mwanadamu alivyowekewa kufa mara moja tu na baada ya kufa akabili hukumu.* (Waebrania 9:27)

Hivyo wanadamu wote wako kwenye mashua ile ile. Wote wamepungukiwa na matarajio ya Mungu, iwe katika mawazo, maneno na hata matendo.

Je, haivutii kuona kuwa katika suala hili kila dini hufuata taratibu za kidini zinazomaanisha utakaso? Kimsingi hizo si zaidi ya ishara za kimfano, na ni wazi kuwa peke yake haziathiri chochote. Huku tukiweza kuisafisha miili yetu kwa nje kwa taratibu hizo za kidini, tunafahamu vyema kwamba hatuwezi

kuondoa dhambi kwa kuosha kwa maji na hivyo kuumba moyo safi!

Yesu aliwahi kutoa kauli nzito sana alipoulizwa kuhusu kutawadha mikono kabla ya kula:

*"Je, hamwelewi kwamba chochote kiingiacho kinywani huenda tumboni, na hatimaye hutolewa nje kikiwa uchafu? Lakini kitokacho kinywani hutoka moyoni, na hiki ndicho kimtiacho mtu unajisi. Kwa maana ndani ya moyo hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wizi, ushahidi wa uongo na masingizio. Haya ndiyo yamtiayo mtu unajisi; lakini kula bila kunawa mikono hakumtii mtu unajisi."*

(Mathayo15:17-20)

Je, haivutii kuona kuwa katika suala hili kila dini hufata taratibu za kidini zinazomaanisha utakaso?

Taratibu za kidini ni ukumbusho tu wa hitaji letu la utakaso - kwa maana tunajua ya kuwa hatuko safi.

Baada ya kutenda dhambi Daudi alionyesha vizuri nia yake kwenye moja ya Zaburi zake:

*Unioshe na uovu wangu wote na unitakase dhambi yangu. Kwa maana ninajua makosa yangu, na dhambi yangu iko mbele yangu daima. Dhidi yako, wewe peke yako, nimetenda dhambi ... Ufiche uso wako usizitazame dhambi zangu, na uufute uovu wangu wote. Ee Mungu, uniumbie moyo safi.* (Zaburi 51:2-4, 9-10)

Nina hakika sisi sote tunakubaliana na tunaguswa na hili. Hata hivyo kwenye mada nyingine nyingi hatuelekei kukubaliana. Tunapojadili mambo ya kiroho ni kawaida kuhoji kulingana na misimamo yetu. Alikuwa sahihi aliyesema kuwa mara nyingi misimamo yetu ni adui wabaya zaidi kwa ile kweli kuliko uongo. Misimamo ni zaidi kidogo ya maoni. Mazungumzo



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 3 13-04-2022 12:22:08

kwenye msingi huu yanatabirika: Kila mtu huzungumza na hakuna anayesikiliza. Tusifuate mwelekeo huo. Ninapendekeza jibu liwe kukabili moja kwa moja na kwa uaminifu mambo yenye ubishani kwa kusudi la kugundua kwa pamoja yale yanayoaminika, na sababu zake. Tukumbuke ni suala linaloathiri hali ya milele! Kwa hiyo tusifanye tu utafiti wa juujuu. Hatutaki kuwa kwenye hatari ya mmoja wetu kupotea njia! Msingi wa imani yetu usipokuwa kwenye ufunuo wenye ushahidi kutoka kwa Mungu, lazima tufanye uhakiki. Maana kama tunaamini na kufuata kweli ya Mungu, tunaogopa tutapoteza nini? Kweli ya Mungu lazima itambuliwe na kutetewa kwa ushahidi. Ni jinsi tunavyoitambua.

Hadi sasa tukiwa tumefahamiana kidogo, nina hakika kuwa, tukiendelea kuwasiliana kwa wema na ufahamu na uamuzi wenye utulivu, kwa pamoja tutakipata kile kinachotuhusu zaidi kuliko kingine cho chote kwenye dunia hii!

Wako kikweli,

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 4 13-04-2022 12:22:08

***Barua ya Pili***

# Uaminifu pekee unatosha?

*Mpendwa Abdallah*

Nilijua nitakuwa sahihi kutarajia kuwa jibu lako litatoka moyoni. Asante!

Ninazitambua hisia zako na sina mashaka na uaminifu wako hata kwa dakika moja. Lazima uaminifu uwe msingi wa mazungumzo yo yote kuhusu Mungu na uhusiano wetu na Yeye. Hata hivyo, lazima uunganishwe kwenye ukweli uliothibitishwa. Lazima tuulize swali hili: Ninayoyaamini kwa dhati ndiyo hasa kweli yenyewe? Mama anaweza kuamini kabisa kuwa mwanawe hana hatia kwa kosa alilodaiwa kufanya. Lakini mwana huyo hana hatia kwa sababu hiyo? Inaonekana si kiwango cha uaminifu wetu kitakacholiamua hilo, bali ni uchunguzi. Uaminifu hauwezi kubadilisha kosa likawa kweli.

Kwa hiyo jambo muhimu si uaminifu wetu bali lengo la uaminifu wetu. Kwa hiyo naomba ukubali kuwa, pamoja na mimi kusifu uaminifu wako, ninataka maelezo zaidi juu ya sehemu ya kile unachoamini kuwa ni sahihi. Ninaeleza.

Unatamka kuwa una mashaka sana kuhusu kuaminika kwa toleo la leo la Biblia. Kwa namna fulani nililitarajia hili, lakini bado linanishangaza! Napenda nijaribu kuyajibu mashaka yako. Kwanza itabidi tutofautishe kati ya yale tuliyo nayo na vile tunavyoyatafsiri. Kile ambacho Uislamu kamwe haujakikubali kilitokea kwenye Ukristo. Kwa karne mbili hivi iliyopita wahakiki wa Biblia, wengi wao wanatheolojia, walichukua uhuru wa kuandika na kueneza uhakiki wao, ambao mara nyingi msingi wake ulikuwa tafsiri za kupita kiasi. Mara nyingi sana hizi huakisi misimamo na maoni yao binafsi wanayoona yanafaa kwa kuyatumia wakiifafanua Biblia. Lakini wapo na



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 5 13-04-2022 12:22:08

wamekuwako wahakiki wengine wenye msimamo tofauti, na tunahitaji kusikiliza wanachosema.

Inabidi tuione tofauti kati ya kile kinachoitwa 'Uhakiki wa Andiko' na ile mbinu ya kuhakiki inayoitwa 'mbinu ya kihakiki ya kihistoria'. **Uhakiki wa Andiko** ni sayansi, iliyoundwa ili kubainisha andiko lenyewe la asili linasema nini, na kuyaondoa makosa yo yote yanayoweza kuingia kwenye andiko lililotunzwa kwa karne nyingi kwenye maandiko yaliyonakiliwa kwa mkono. Sayansi hiyo hujaribu pia kusahihisha kama kuna maneno, vifungu vya maneno au tamadhali za usemi vinavyoeleweka kwa namna isiyo sahihi. Wasomi wengi, Wakristo na wengine, wamechunguza kwa makini na kikamilifu kila andiko la zamani. Hili lilisaidia kutambua kama kuna kosa lo lote na kuangalia lilikoanzia. Hili hutuhakikishia kuwa leo tuna nakala iliyo karibu na ukamilifu ya ufunuo wa asili.

**'Mbinu ya kihakiki ya kihistoria'** ni ya hali tofauti kabisa. Hiyo hujaribu 'kusahihisha' andiko kwa kukadiria uwezekano wa habari zake, kama ninaweza kuliweka hivi. Kwa mfano, Biblia hufundisha kuwa Wayahudi waliivuka Bahari ya Shamu wakiwa kwenye nchi kavu, au kuwa Yesu alizaliwa na bikira, na alitembea juu ya bahari na alifufua wafu wakawa hai. Kwa kuwa hilo haliwezekani, wahakiki wanaotumia mbinu hiyo huona kuwa lazima kuainisha andiko la aini hiyo kuwa kisasili, yaani, hadithi ya kubuni. Kwa njia na namna tofauti kalamu zao zimeiondolea Biblia lo lote lisilo la kawaida. Kama inavyotarajiwa, uhakiki wao kwa kiasi kikubwa ulichangia hali ya kiroho kudhoofika katika ulimwengu wa Magharibi. Kwa njia hii Mungu alifutwa kwenye akili za watu wengi. Kwa kukusudia au bila ya kukusudia, wahakiki hawa walizifanya akili zao wenyewe zenye ukomo kuwa hakimu juu ya Mungu asiye na ukomo, wakikadiria na kuweka masharti kwa anachoweza na asichoweza kufanya. Hili llilitokeza ufafanuzi ulio wa kibinadamu sana wa Kitabu cha kimungu na mwandishi wake. Hiyo tunaiita 'elimu isiyoendeshwa na dini'. Ni hali ya



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 6 13-04-2022 12:22:08

kuhuzunisha, ila imekuwa namna ya fikira inayotawala kama inavyoonyeshwa na vyombo vya habari vya Kimagharibi.

Katika kuunga mkono hoja zao, wahakiki hawa walifikiria tena tarehe za vitabu vya Biblia, wakidai, kwa mfano, kuwa Torati ya Musa iliandikwa na Ezra, aliyeishi miaka 900 baada ya Musa. Hili lilitokana na dhana kuwa uandishi haukujulikana wakati wa Musa. Sasa tunajua kuwa kabla ya Ibrahimu (miaka 500 kabla ya Musa), uandishi ulikuwa zoezi la kawaida.

Huku tukiwa tayari kutambua makosa ya nakala yanayoweza kutokea, tuna hakika kabisa kuwa haya hayataathiri wala kubadilli ujumbe na muktadha wa Neno la Mungu.

Baadhi ya wahakiki hudai pia kuwa baada ya kifo cha Yesu, Paulo alikuja akauteka nyara Ukristo (kupaa kwa Yesu walikufuta wakiona kuwa ni jambo lisilowezekana, na hivyo habari hiyo ni hadithi ya kubuni). Paulo alikuja akauteka nyara Ukristo. Inadaiwa kuwa aliiondoa Injili ili aweke theolojia yake. Lakini kumbukumbu za wakati ule huonyesha wazi kabisa kuwa kamwe hakukuwa na ubishani wa kimafundisho kati ya Paulo na mitume wengine wa Yesu. Kwa kweli alishauriana nao.

Tuko tayari kukubali makosa ya mara moja yaliyotokea wakati wa kunakili, lakini tuna uhakika kabisa kuwa haya hayawezi kwa namna yo yote kuathiri au kuvuruga ujumbe na yaliyomo kwenye Neno la Mungu. Kwa kweli tunaona ni muujiza, kwamba maandiko ya Biblia, yaliyonakiliwa kwa mkono kwa vipindi vya hadi miaka 3000, yakiwa barabara kabisa.

Inatushangaza kuwa Waislamu wengi huzitumia hoja hizi za kidunia kueneza dhana ya kuzibatilisha Injili, huku wakikataa kutumia uhakiki wa andiko unaohitajika sana kwenye maandiko yao wenyewe. Wanaupuuza kabisa ukweli kuwa ingawa Kurani ni ya karibuni zaidi, ina matatizo kama hayo au

hata magumu zaidi. Ninautambua ukubwa wa kauli hii, lakini haiwezi kukuchukiza kama zinavyotuchukiza kauli za Kiislamu kuhusu Biblia. Kwa ufupi, ninapendekeza sisi sote tutumie kanuni hizohizo tunapojadiliana jambo hili. Madaktari wa Kislamu wanaotangaza kuwa Biblia ilipotoshwa nao hawauoni ukweli kuwa wanatheolojia maarufu zaidi wa Kiislamu kama at-Tabari (aliyekufa mwaka wa 855 baada ya Kristo), pamoja na al-Ghazzali (aliyekufa mwaka wa 1111 baada ya Kristo) waliuamini uhalisi wa andiko la Injili (ya Kigiriki). Na huo ndio ujumbe inaoukuza Kurani:

> "Semeni ninyi: Tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa, na yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu, na Ismaili na Ishaqa na Yaaqubu na kizazi, na waliyopewa Musa na Isa, na pia yale waliyopewa manabii wote kutoka kwa Mola wao: **hatutofautishi baina ya yoyote katika hao."** (Surah al-Baqara 2:136)

> "Na Tukawafuatishia Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati na Tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongozi na nuru, na uwongozi na mauidha kwa wamchao ... na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio waasi. **Watu wa Injili wahukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu ndani yake. Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio waasi.** Basi wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao." (Surah Mâ-ida 5:46, 47, 48)

> "Na semeni: Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu." (Surah al-Ankabût 29:46)

Ni wazi kabisa kuwa wakati Kurani ilipoandikwa, hakukuwa na dokezo lililotolewa po pote kuhusu kuvurugwa au kutoaminika kwa Biblia. Ye yote anayeipinga sasa siyo tu atakuwa anaipinga Kurani, bali pia itabidi ayajibu maswali kama: NI NANI



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 8 13-04-2022 12:22:09

aliyeibadilisha au kuiharibu Biblia? Biblia ilipotoshwa LINI? IKO WAPI nakala ya asili, au ushahidi unaoonyesha kuwa ilikuwako nakala ya asili kama hiyo ya kutofautiana na kweli iliyopo? Hadi sasa sijasikia jibu kwa maswali haya.

Kama Biblia ilipotoshwa kabla au wakati wa Muhammad, Kurani haingeizungumzia Biblia kwa namna chanya hivyo.

Kama Biblia ilipotoshwa kabla au wakati wa Muhammad, Kurani haingeizungumzia Biblia kwa namna chanya hivyo. Kama Biblia ilibadilishwa au kupotoshwa baadaye, maandiko mengi ya zamani yaliyopo, ambayo ni ya kabla ya wakati wa Muhammad kwa mamia ya miaka, yangethibitisha kama kuna ukweli kama huo. Aidha tuliona sasa hivi kwenye Kurani kuwa Biblia ni Neno la Mungu. Inabidi tuongeze, pia kutoka kwenye Kurani kuwa, **Hakuna anayeweza kuyabadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu** (Surah 6:34 na 10:64). Kwa hiyo, wahakiki wa Biblia wa Kiislamu wanajaribu kufanya nini?

Baadhi ya Waislamu huhoji kuwa Kurani inasema wazi kwamba Biblia ilibadilishwa. Hunukuu:

> "Enyi mliopewa Kitabu! Mbona mnachanganya haki na batili, na mnaficha haki, hali mnajua?" (Surah Al-Imran 3:71)
>
> "Na miongoni mwao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) Kitabu ili mpate kuyafikiri maneno yao kuwa ni ya Kitabu wala si ya Kitabu." (Surah Al-Imran 3: 78)

Vifungu hivi vinasema tu kuwa Biblia, kama ilivyotolewa na Wayahudi kwa umma, kama muktadha unavyoashiria, ilibadilishwa kwa **ndimi zao** si kwa kalamu zao. La sivyo Kurani haingependekeza kuwa Waislamu wawaulize watu wa Kitabu kuhusu yaliyomo ya Biblia:

> "Basi waulizeni wenye kumbukumbu." (Surah al-Anbiya, 21:7)



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 9 13-04-2022 12:22:09

Tunaweza kuuliza, kwa nini Waislamu wengi hivyo wanaamini kuwa Biblia ilipotoshwa, huku hili likikanushwa na historia, wachunguzi wa mambo ya kale na Kurani. Jibu linaonekana kuwa ni njama.

... kwa nini mtu ye yote na kwa sababu yo yote, ajaribu kulibadilisha Neno la Mungu?

Ibn-Khazem (aliyekufa mwaka wa 1064 bK) alitawala kusini mwa Spain kwa muda fulani kama kaimu mtawala wa Calipha. Alipokuwa akiisoma Kurani alikutana na aya iliyomwonyesha Yesu akizungumzia Habari Njema ya Mtume atakayekuja baada yake na ambaye jina lake ataitwa Ahmad (Surah 61:6). Maana ya neno hili la Kiarabu inafanana na maana ya jina 'Muhammad'. Lazima alikuwa amesoma pia kuhusu "nabii asiyejua kusoma wala kuandika (yaani Muhammad) anayetajwa kwao, kwenye Taurati na Injili" (Surah 7:157). Hivyo alianza kuitafuta Biblia aone vidokezo hivi kuhusu Muhammad. Huenda alishangaa maana hakuviona. Alichokiona, lakini, ni kwamba kuna tofauti nyingi kati ya vitabu hivyo viwili, vyote vikidhaniwa kuwa vimetoka kwenye chanzo kimoja cha kimungu. Tunaweza kuliona tatizo alilokuwa akilikabili ibn-Khazem. Biblia na Kurani vyote hudaiwa kuwa ni Neno la Mungu – na vinapingana.

Uamuzi wa Ibn-Khazem ulikuwa kutokuhoji ukamilifu wa Kurani. Alichagua kusadiki kuwa kwa kuwa Injili inapaswa kukubaliana na Kurani, na kwa sababu Muhammad alikuwa ameizungumzia vema, basi lazima Injili iliyopo iwe imebatilishwa na Wayahudi na Wakristo. Dhana hii inaweza kuonyesha hamasa yake kwa Kurani, lakini msingi wake si ukweli wa kihistoria.

Tangu wakati huo Waislamu wamehoji ukamilifu wa Biblia. Hoja yao haipingwi na Kurani tu, bali pia na wachunguzi wa mambo ya kale na hoja za historia zenye nguvu zinazozidi



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 10 13-04-2022 12:22:09

kuongezeka, zinazounga mkono uhalisi wa Biblia. Na zaidi, kwa nini mtu awaye yote na kwa sababu yo yote ajaribu kulibadili Neno la Mungu?

Huenda barua hii imekusaidia kupata picha fulani ya kile ambacho inaonekana Waislamu walio wengi hawakijui. Wakristo wa kweli wana nafasi maalumu sana kwa ajili ya Biblia mioyoni na maishani mwao. Ni barua ya Mungu ya upendo kwao.

Kwa sababu inaweza kuumiza hisia zako, ni juhudi inayoniumiza kukuandikia barua inayohoji chanzo cha misimamo yako ya ndani. Lakini naamini kuwa hangaiko letu la kufahamu msingi wa imani yetu katika Mungu litatuwezesha kushinda vikwazo vya kihisia.

Ninatumaini na kuamini kuwa barua hii inakukuta ukiwa katika hali na afya njema. Tafadhali nijibu mapema!

Salamu za upendo kabisa!

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 11 13-04-2022 12:22:09

*Barua ya Tatu*

## Imeandikwa – na Ilitokea

*Mpendwa Abdallah*

Asante kwa barua yako isiyoficha kitu. Asante pia kwa kunishirikisha unavyomfahamu Nabi Isa, kama unavyomwita Yesu kwenye lugha yako ya kiibada. Siyo tu jina tofauti bali pia nafasi tofauti aliyowekewa kwenye Kurani na kwenye Biblia inayofanya utambuzi wako na hatimaye ufahamu wako kwa Yesu uwe tofauti na wetu. Ulinifanya nitambue hisia zako ambazo wakati mwingine ni kali kuhusu mafundisho ya Biblia yanayomhusu huyo Yesu. Kwa kawaida kwa kiasi kikubwa utambuzi wetu huamuliwa na taarifa tulizo nazo. Tutafanya vema tukichunguza kwa uangalifu tegemeo la vyanzo vyetu vya taarifa ili tuweze kutofautisha kati ya kile ambacho ni halisi – na ambacho ni hadithi ya kubuni.

Ninaona kwanza kabisa tutafute ishara itakayotuhakikishia asili ya kimungu ya hivi 'vitabu vitakatifu' tulivyo navyo. Haielekei ye yote kati yetu kutilia shaka kuhusu Maandiko aliyo nayo kama yamevuviwa na Mungu na hivyo ni ufunuo kutoka Kwake. Lakini kwa kuwa Kitabu chako na Kitabu changu hutofautiana kwenye mambo muhimu, nategemea utakubali kwamba haviwezi vyote kutoka kwenye chanzo kimoja. Chukua kwa mfano kusulubiwa na kufa kwa Yesu. Tukio hili hushuhudiwa wazi wazi na kwa wingi kwenye Biblia, lakini, kwa sababu fulani, linakanushwa na Uislamu. Haiwezekani mitazamo yote kwa pamoja kuwa ni ya kweli. Ningependa uikabili mada hii kwa uwazi na umakini. Inaelekea kuwa nitakutambulisha jambo ambalo hujalizoea.

Mtu ye yote anawezaje kuwa na uhakika kuwa Kitabu kimetoka kwa Mungu, au kama huenda ni andiko lililoandikwa kwa kusudi jema na mtu anayetaka kufanyia mageuzi jamii iliyofifia?

Wakristo wanaamini kile alichokifunua Mungu katika Biblia, kwa sababu inabeba alama ya uanzishaji Wake. Hapa ninazungumzia matukio yasiyotabirika kabisa, ambayo yalitabiriwa na manabii kwenye Biblia, na yaliyotimia mamia ya miaka baadaye. Kwa kweli tunaambiwa wazi wazi mara kwa mara kuwa nabii ambaye unabii wake hautimii asiaminiwe wala kutumainiwa:

> *Mnaweza kuulizana wenyewe, "Tutawezaje kujua wakati ujumbe haukusemwa na* Bwana*?" Ikiwa kile nabii anachotangaza kwa jina la* Bwana *hakikutokea au kutimia, huo ni ujumbe ambao* Bwana *hakusema. Nabii huyo amesema kwa ujuaji. Msimwogope huyo.*
>
> (Kumbukumbu 18:21-22)

> *Hakika* Bwana *Mwenyezi hatafanya neno lolote bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.*
>
> (Amosi 3:7)

Na Mungu alizungumza kupitia kwa Isaya:

> *Kwa hiyo nilikuambia mambo haya tangu zamani, kabla hayajatokea nilikutangazia ili usije ukasema, 'Sanamu zangu zilifanya hayo.'* (Isaya 48:5)

> *"Mimi ni* Bwana*, niliyeumba vitu vyote, ... niyathibitishaye maneno ya watumishi wake, na kutimiza utabiri wa wajumbe wake."* (Isaya 44:24, 26)

Tunaweza kugundua mambo matatu makuu ya unabii kwenye Biblia. La kwanza, unabii hutabiri historia ya kipekee sana ya Wayahudi, hadi kwenye wakati huu. La pili, unabii huuonyesha wakati wa mwisho wa dunia hii kwa kina na kwa hali ya kuvutia, na la tatu, unabii hutabiri, tena kwa kina, maisha ya Masihi Yesu. Kwa maelezo yenye ishara manabii pia waliyatabiri mateso yake na kifo chake msalabani, kadhalika na na vilevile kufufuka kwake katika wafu. Haya kama hayangetimia, tungeweza kuwa na sababu ya kuuhoji ujumbe na kukihoji chanzo cha kimungu cha Kitabu chetu. Lakini unabii huo wote ulitimia isipokuwa



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 13 13-04-2022 12:22:09

ule unaoelezea mwisho wa dunia. Hili hutupa ujasiri wa kuutegemea ujumbe wa Biblia, maana hakuna mtu ambaye angeweza kuyatabiri haya matukio ya kihistoria. Ni Mungu tu ambaye angeweza kuyajua na kuyafunua.

Inavutia basi kusoma mara nyingi kwenye Injili ikisema “kama ilivyoandikwa”, au “kama alivyosema nabii”. Kwenye Agano Jipya tunasoma:

> *Kwa maana yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa kwanza: Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemavyo Maandiko, ya kuwa alizikwa na alifufuliwa siku ya tatu,* ***kama yasemavyo Maandiko****, na kwamba alimtokea Kefa, kisha akawatokea wale kumi na wawili* [Mitume wa Yesu]. *Baadaye akawatokea wale ndugu waumini zaidi ya 500 kwa pamoja, ambao wengi wao bado wako hai, ingawa wengine wamelala* [wamekufa]. (1 Wakorintho 15:3 - 6)

Maneno “kama yasemavyo Maandiko” yanamaanisha yale yaliyoandikwa na manabii waliokuwa wakiishi mamia ya miaka kabla. Ni Maandiko haya yaliyotimizwa ndani ya Yesu.

Walitoa taarifa kuhusu wakati na mahali atakapokuja (Mika 5:2, Danieli 9:24 nk - kifungu hiki kinahitaji msaada wa kiutangulizi ili kieleweke); kuwa atazaliwa na bikira (Isaya 7:14), na litakavyokuwa jina lake (Isaya 63:8 - Mwokozi kwa Kiebrania ni Yeshua; hili ndilo jina alilokuwa nalo hasa Yesu akiwa duniani). Pia uungu wake ulitabiriwa (Isaya 7:14 na 9:6 - jina Imanueli lina maana ya Mungu pamoja nasi) na yote yalifikia kilele katika unabii uliotabiri kusulubiwa na kufa kwake. Niruhusu nitaje utabiri mchache kuhusu hayo. Daudi aliandika kuhusu Yesu kama mwaka wa 1000 kK akisema:

> *Mbwa wamenizunguka, kundi la watu waovu limenizingira,* ***wametoboa mikono yangu na miguu yangu.*** *Naweza kuhesabu mifupa yangu yote, watu wananikodolea macho*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 14 13-04-2022 12:22:09

*na kunisimanga. Wanagawana nguo zangu wao kwa wao, na vazi langu wanalipigia kura.* (Zaburi 22:16 - 18)

Mwaka wa 700 kabla ya Kristo Nabii Isaya alisema:

*Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye mateso. Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulidhania kuwa amepigwa na Mungu, akapigwa sana naye, na kuteswa. Lakini* ***alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu****, alichubuliwa kwa ajili ya maovu yetu;* ***adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake****, na* ***kwa majeraha yake sisi tumepona****.*

*Sisi sote, kama kondoo, tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe, naye* ***Bwana aliweka juu yake maovu yetu sisi sote****. Alionewa na kuteswa, hata hivyo hakufungua kinywa chake;* ***aliongozwa kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni,*** *kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya wao wamkataye manyoya, hivyo hakufungua kinywa chake. Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa. Nani awezaye kueleza kuhusu kizazi chake? Kwa maana alikatiliwa mbali na nchi ya walio hai,* ***alipigwa kwa ajili ya makosa ya watu wangu****. Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu, pamoja na matajiri* ***katika kifo chake****, ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake ... Kwa maarifa yake, mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki, naye* ***atayachukua maovu yao ... Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi, na kuwaombea wakosaji****.* (Isaya 53:3 - 12)

Mtu yeyote mwaminifu anaweza kuupuuza au kuuweka kando au ‘kuuelezea’ vinginevyo ushahidi kama huu?

Unabii huu wote ulitimia. Hili hutupa imani ya kuutegemea ujumbe wa Biblia.

Ili kulikuza hili zaidi, Biblia



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 15 13-04-2022 12:22:09

ina habari nyingi za walioona kwa macho yao, ambazo zingekataliwa na watu wa wakati ule kama hazikuwa za kweli. Fikiria kwa mfano, Wayahudi wangefanyaje, kama Petro, mmoja wa wanafunzi wa Yesu, angesema uongo alipowahutubia, wiki saba baada ya Yesu kusulubiwa, akitamka:

> *"Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya nisemayo: Yesu wa Nazareti alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa miujiza, maajabu na ishara, ambayo Mungu alitenda miongoni mwenu kupitia kwake, kama ninyi wenyewe mjuavyo. Huyu mtu akiisha kutolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa kwa kujua kwake Mungu tangu zamani, ninyi, kwa mikono ya watu wabaya,* ***mlimuua kwa kumgongomea msalabani****. Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu akamwondolea uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana yeye kushikiliwa na nguvu za mauti."* (Matendo 2:22-24)

Wayahudi wangefanyaje, kama Yesu hangesulubiwa au kuuawa? Wangelikataa hilo kwa nguvu. Lakini hakuna aliyelihoji hili, kwa sababu wote walijua kilichotokea. Huku Wayahudi wakidai wakati wote kuwa Yesu siye Masihi, kamwe hawakukikanusha kifo chake msalabani. Na walijua kuwa lilitokea, maana walikuwako kwenye tukio.

Niongeze tu ushahidi mmoja zaidi wa kuzingatiwa, ambao unategemeza uaminifu wa habari ya kusulubiwa kwa Yesu kwenye Injili. Tunatambua kuwa maisha ya Yesu kwenye eneo la mbali kama la Uyahudi hayakuwa na umuhimu kwa wanahistoria wa Kirumi wa wakati wake, walioandika habari za vita na washindi. Hata hivyo mwanahistoria mashuhuri zaidi, Cornelius Tacitus, akiwa mpinzani mkali wa Ukristo wa mwanzo, aliandika miongoni mwa mambo mengine:

> "Jina 'Mkristo' hutokana na Kristo, aliyeuawa chini ya utawala wa wakili Pilato" (Kumbukumbu za Historia 15.44).

Flavius Josephus alikuwa jenerali wa Kiyahudi, aliyepigana



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 16 13-04-2022 12:22:09

vita vya mwisho kwa ajili ya Yerusalemu dhidi ya Warumi (mwaka wa 70 bK). Alichukuliwa kama mfungwa akawa mwanahistoria wa Kirumi kwa ajili ya Israeli. Aliishi muda mfupi baada ya wakati wa Yesu, na aliandika:

> "Sasa, si zamani sana alikuwako Yesu, mtu mwenye hekima, kama ni halali kumwita mwanadamu, maana alikuwa mtenda maajabu, mwalimu wa watu wanaoipokea kweli kwa furaha. Aliwaleta kwake Wayahudi wengi na watu wengi wa Mataifa. Alikuwa (huyo) Kristo. Na Pilato akishauriwa na wakuu kati yetu, alipomhukumu asulubiwe msalabani, wale waliompenda mwanzoni hawakumwacha; maana alionekana kwao akiwa hai tena siku ya tatu; kama manabii wa kimungu walivyokuwa wameyatabiri haya na mambo mengine elfu kumi ya ajabu kuhusu yeye."
>
> (Antiquities of the Jews)

Ushahidi muhimu kama huo lazima iliwepo sababu ya kuutoa. Na bila shaka huyo ni Mungu akishughulika audhihirishe ujumbe wake kwa vizazi vijavyo, kwa wale watakaotegemea namna fulani ya uthibitisho wa kuonekana au ushahidi ili waamini aliyoyafunua.

Kwa nini ninaandika yote haya? Kwa nini ninahatayarisha kuvuruga amani na upatanifu kati yetu? Ninatumaini umeligundua hilo kwa sasa: ni kwa sababu ninakujali! Hadi sasa huenda hujaitambua haja ya kuuthibitisha msingi wa imani yetu. Walio wengi duniani hufuata dini zao wakiamini kwa moyo safi kuwa mambo yote yako sawa na kuwa wanafuata njia sahihi.

Hata hungetaja vipingamizi hivi kwenye Biblia bila ya wewe kuhoji uadilifu wake na kuaminika kwake, na bila ya kuvutiwa kufanya hivyo. Kwa hiyo inabidi nikuhamasishe kuijaribu misingi ambapo hatima yako ya milele inakaa.

Hadi sasa huenda hujalitambua hitaji la kuuthibitisha msingi wa imani yetu.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 17 13-04-2022 12:22:09

Lazima ufahamu kuwa sikuandikii barua hii ili kuiharibu imani yako katika Mungu, bali zaidi sana kwa sababu ningependa kuifanya nzuri zaidi na kuiimarisha. Hili huhitaji uchunguzi makini.

Jana mke wangu na mimi tulitaka kumtembelea mtu hospitalini. Jamaa fulani akaelezea njia ya kufikia huko, kwa usahihi kabisa – ila alikosea kidogo tu. Kwenye kona moja tuliambiwa tugeukie kushoto badala ya kugeukia kulia. Kwa bahati nzuri niliiangalia njia kwenye ramani nikaligundua kosa. Bila ya kuangalia tusingefika tulikotaka kufika. Wakati mwingine hili huwa si muhimu sana, lakini likihusisha hatima ya milele, ni muhimu sana.

Nina hamu sana kusikia maoni yako na ninatarajia jibu lako mapema. Ninakusalimu kwa upendo kabisa!

Wako wa kweli,

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 18 13-04-2022 12:22:09

***Barua ya Nne***

## Ukweli na Hisia

*Mpendwa Abdallah*

Si lazima nikuambie nilivyoifurahia barua yako ya mwisho. Ni vizuri kuwa uhusiano wetu binafsi uko wazi kiasi hicho bila kujali kwamba imani zetu ziko kwenye misingi inayotofautiana. Nimefurahi kuwa unaonekana kukubaliana na haja ya kuyaendea masuala ya kiroho kwa busara na utulivu na kuitambua hoja inayowakilishwa na unabii uliotimia, ambayo kwa msomaji mwaminifu inaonekana kuwa wazi na ya kusadikisha. Kadhalika na taarifa za mashahidi walioona na vyanzo vya kihistoria. Kwa pamoja huo ni mwamba ambapo tunaweza kujenga imani yetu kwenye Biblia tukiwa na usalama.

Huku ni vema kuwa na maisha ya kimhemko, haipasi mazungumzo yetu ya kiroho kutawaliwa na mihemko pekee. Lazima tuuangalie ukweli pia. Nyakati nyingine hilo linaweza kuumiza. Ndiyo maana tunafundishwa katika Biblia tuwe *tukiambiana kweli kwa upendo* (Waefeso 4:15). Yuko sahihi aliyesema kuwa ukweli bila ya upendo una ukatili, na upendo bila ya ukweli ni kuingiliwa na mihemko. Kama vile mihemko inavyopaswa kujengwa kwenye uhalisi, ndivyo kweli inavyopaswa kuambatana na upendo. Vinakaa pamoja.

Kwenye barua yako unaonyesha pia mtazamo unaokubaliwa na karibu Waislamu wote, kuwa Kurani ilivyo sasa inafanana na ile ya asili. Mapokeo ya Kiislamu ya tangu wakati wa Makhalifa wa mwanzo hayakubaliani na dhana hii, jambo ambalo kila msomi aliyesomea ni **lazima** ajue na atambue.

Kwenye barua yako unataja sababu tatu kwa nini unaamini kuwa Kurani ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Ninalichukulia hilo kwamba unaziorodhesha hizi sababu kama jibu lako kwa ushahidi wa uvuvio wa Biblia.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 19 13-04-2022 12:22:09

Kama nimekuelewa vizuri, unamaanisha kuwa ushahidi mwingine nao unaweza kuthibitisha ufunuo wa Mungu. Kwanza, unalenga kwenye ubora wa kimaandiko na yaliyomo kwenye Kurani. Pia unaona kuwa Waislamu wengi kuweza kuikariri Kurani nzima ni muujiza, hivyo huonyesha asili yake ya kimungu. Tatu, unatamka pasipo shaka lo lote kuwa kamwe Kurani haijaingiliwa, bali kila kipengele kimehifadhiwa kama kilivyotoka kwenye mdomo wa Mtume.

Kama vile mihemko inavyopaswa kujengwa kwenye uhalisi, ndivyo kweli inavyopaswa kuambatana na upendo. Vinakaa pamoja.

Ye yote aliye na ujuzi wa msingi kuhusu lugha ya Kiarabu hatakuwa na tatizo kuusifia uzuri wa kishairi wa angalau sura za mwanzo za Kurani za Mecca. Hata hivyo kuhusu kisarufi na kuchagua maneno inasemekana kuwa Kurani ya Kiarabu haionekani kuwa na kiwango kamili. Lakini hata ingekuwa nacho, lazima tutambue kuwa ni vema kuona kuwa hata mazao yaliyo bora kabisa ya werevu wa mwanadamu, bado ni ya kibinadamu. Uthibitisho wa ishara ya kimungu - kama unabii uliotimia, ingekuwa ubora wa Kurani juu ya kile anachoweza kuzalisha mwanadamu.

Kuhusu yaliyomo kwenye Kurani, bila shaka Wakristo huilinganisha na Injili. Katika uaminifu wote, na tukijaribu kuwa wa haki na bila upendeleo iwezekanavyo, itabidi tukiri kuwa tunaipendelea Iinjili. Itakuwa nje ya nafasi inayopatikana katika barua kama hii kutoa sababu za maoni haya hapa sasa, lakini ningependa kukutia moyo usome kwenye Agano Jipya - huku na mimi nikisoma kwenye Kurani. Huenda usome tu, kwa mfano, Injili kama ilivyoandikwa na Yohana, kuanzia sura ya 10 na kuendelea, au kwenye waraka wa kwanza kwa Wakorintho sura ya 13, nk.

Kukariri Kurani ni jambo lingine kabisa. Nakumbuka niliwaangalia makumi ya vijana wakiwa kwenye uwanja wa



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 20 13-04-2022 12:22:09

Chuo Kikuu cha al-Azr cha Cairo, wakiikariri Kurani. Uwezo wa kufikiri, bidii, na huenda kumbukumbu kama ya kupiga picha, huchangia hapa. Kwa mfano, ungekuwa muujiza kama ufahamu huo ulipatikana mara moja, bila ya mafunzo yo yote.

Lakini acha nirudi kwenye wazo lako kuu, kuwa Kurani imehifadhiwa katika utimilifu wake. Haiwezekani kujumuisha kauli zangu zote kwenye barua fupi kama hii, lakini nitafanya hivyo kwa furaha ukipenda. Naungwa mkono na mapokeo ya Kiislamu kuwa wakati wa uhai wa Muhammad zilikuwako 'namna' saba tofauti za Kurani:

Muhammad alisema, "Kurani hii ilifunuliwa kwa namna saba, kwa hiyo karirini iliyo rahisi zaidi!". (Al-Bukhari juzuu ya VI, Uk. 482, Sura ya LXI (5) Dhidi ya 514, Mishkatul Masabih juzuu ya 3, uk.702-704; Tafsiri ya at - Tabari na Sherehe ya al - Baidawi).

Imependekezwa kuwa hili lina maana ya lahaja tofauti. Lakini haiwezekani kuwa hivyo. Lina maana ya maandiko tofauti.

Lazima pia tutambue kuwa toleo la Kurani la Uthmani kwa kweli ni tokeo la upitiaji upya wa maandiko ya mapema. Mbali na toleo la Kurani, lililokusanywa na kupangwa kwa taratibu na Zaid b. Thabith kwa pendekezo la Abu Bakr na Umar, yalikuwako maandiko mengine mengi, yaliyounganishwa na watu wenye vipawa vizuri hata kuliko Zaid kama vile Abdallah b. Mas'ud, Ubay b.Ka'b na Abu Moosa.

Kupitiwa upya Kurani kuliagizwa na Uthman, kwa sababu makusanyo tofauti ya maandiko ya Kurani yalishindana. Baada ya mapitio ya Uthmani kukamilika, matoleo yote ya nyuma yalichomwa moto. Hata nakala iliyoandaliwa na Zaid, ambayo wakati huo alikuwa nayo Hafsa, mjane wa Muhammad, iliharibiwa (na Marwan ibn-al-Hakam, Gavana wa Medinah) (al-Bukhari juzuu ya VI, ukurasa wa 477-479; Sura ya LXI3 dhidi ya 509, Mishkatul Masabih juzuu ya 3, Ukurasa wa 664, Masahif iliyoandikwa na Ibn Abi Dawood, kurasa za 24, 25, na ibn Asakir, dhidi ya 445).

Sasa, hilo ni jambo kubwa mno la kufanya: Ni kuondoa na kuharibu ushahidi! Hata hivyo tumefurahi kusema kuwa, kwa kuwa maandiko haya ya mwanzo yalikaririwa na watu wengi, yameendelea kuwako kwenye majadiliano ya kitheoloja yaliyoandikwa, na yanaweza kulinganishwa na toleo la Uthman. Kando na tofauti nyingi ndogo ndogo, baadhi ya maandiko hayo yalikuwa na Surah au Aya nyingi zaidi ya mengine. Tunaona pia maandiko yaliyoondolewa, yaliyobadilishwa na yaliyoongezwa (Masahif iliyoandikwa na Ibn Abi Dawood, kurasa za 24, 25, na ibn Asakir, dhidi ya 445). Na makusanyo ya Ibn Abu Dawood ya hivi vifungu vya Kurani vinavyotofautiana hujaza kurasa mamia kadhaa.

Tukilitambua hili, pamoja na kuwa na moyo unaoamini tuongeze akili ya kiuhakiki ambayo pia ni wazi. Akili ya kiuhakiki ila si kwa Mungu - maana sisi ni nani hata tumhoji? Lakini ni kwa mwanadamu na madai yake!

Ninakusihi tena usiyaone ninayokuandikia kuwa ni tusi. Siandiki haya ili kukukasirisha au kukuumiza. Kinyume chake, ninataka siyo tu wewe bali *watu wote waokolewe na wafikie kuijua kweli* (1 Timotheo 2:4), kama Biblia inavyosema.

Wako wa kweli,

*Theofilo*

## *Barua ya Tano*

# Biblia, Kurani na Sayansi

*Mpendwa Abdallah*

Asante kwa jibu lako la haraka na roho uliyokuwa nayo wakati wa kuandika. Inaonekana tunahusika sana!

Kwenye barua yako unaleta hoja kutoka kitabu cha "Biblia, Kurani na Sayansi" kilichoandikwa na Maurice Bucaille. Unaandika kwamba ndani ya kitabu hicho ya kimungu ya Kurani inashuhudiwa sana.

Kuileta sayansi kwenye picha ni mwelekeo mpya katika miongo michache iliyopita. Baadhi ya wasomi wa Kiislamu huiona hii kuwa ushahidi wa chanzo cha kimungu cha Kurani. Wanadai kuwa ujuzi fulani wa kisayansi ambao haukujulikana wakati wa Muhammad, unaakisiwa kwenye Kurani. Hasa ufahamu wa sasa wa kiinitete (mimba) kuthibitisha wazi inayoyasema Kurani kuhusu mada hii. Kuumbwa kijiolojia kwa ulimwengu, ukijumuisha dunia, ni mada nyingine. Kwa hali hiyo, nakubali ungeweza kuwa ushahidi wenye nguvu kwa uvuvio wa Kurani, lakini sivyo.

Dr. Bucaille anaona kwenye Kurani maelezo kuhusu asili ya ulimwengu ambayo anavyoona yeye, mwanzoni ilikuwa gesi iliyosababisha 'Mshindo Mkubwa', uliofanikisha kuundwa kwa makundi ya nyota na mifumo ya jua, ukijumuisha jua letu na sayari zake (uk.139). Hili hutokana na anavyotafsiri kwa ubunifu vifungu viwili vya Kurani ambapo tunasoma:

> "Je! Hawakuona wale waliokufuru ya kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana, kisha Tukaviambua" (Sura 21:30) na
>
> "Kisha Akazielekea mbingu na zilikuwa moshi, Akaziambia (mbingu) na ardhi: Njooni ..." (Surah 41:11).



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 23 13-04-2022 12:22:09

Vifungu vya Kurani vyenye usambamba vinapendekeza jambo tofauti. Vinataja nguzo zinazozuia mbingu zisiiangukie dunia:

> "Mwenyezi Mungu..... amezishikilia mbingu zisianguke juu ya ardhi" (Surah 22:65).

> "Ameziumba mbingu pasipo nguzo mzionazo; Ameiweka milima katika ardhi Ili isikusukenisukeni" (Surah 31:10).

> "Mwenyezi Mungu ndiye Aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnaziona hivi" (Surah 13:2).

Vifungu hivi vinaashiria kwa kusadikisha kuwa Kurani haizungumzii "Mshindo Mkubwa" bali inajaribu kuelezea kwa nini anga haliiangukii dunia.

> Pamoja na nia chanya zaidi duniani zingehitajika fikra nyingi sana kuwezesha aya hizi kueleza kazi ya ulimwengu wetu.

Kwenye vifungu vile vile inadaiwa kuwa uwiano wa Sheria ya Mvutano na Nguvu ya Mwendo wa nje (Centrifugal Force) ndani ya mfumo wa jua unaelezewa na vifungu hivi (uk. 152 nk). Mvutano wa sayari ya mbingu kulingana na Kanuni ya Asili, huvutia vitu vingine vyote viielekee. Bila shaka hilo lingeuondoa uwepo wa sayari hiyo. Lakini nguvu ya uvutano imewianishwa na nguvu ya mwendo wa nje kutokana na mwendo wa sayari ikilizunguka jua. Kama mpira ulioning'inizwa ukizungukia ncha ya uzi, unavyozuiwa usiondoke, vivyo hivyo sayari hulazimishwa na nguvu ya mwendo wa nje uwe mbali na jua, lakini hubakia zilipo kwa sheria ya mvutano. Kwa hiyo uwiano kati ya nguvu zinazopingana huziweka sayari zikizungukia mzingo wake. Ninafikiri ni Isaac Newton aliyezigundua Sheria hizi kwenye karne ya 17. Je, tunaziona kweli hizi Sheria za Asili, moja kwa moja au kwa ishara, zikitajwa kwenye Kurani kwa ujumla au hasa kwenye aya hizi zilizotajwa? Kwa kweli si kwenye vifungu hivyo vilivyotajwa. Na Isaac Newton angeliweza kuzieleza kwa



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 24 13-04-2022 12:22:09

usahihi hizi Sheria za Asili kama alivyofanya kwa kuangalia ufahamu wa vifungu hivyo? Nina hakika tunakubaliana kuwa pamoja na nia chanya zaidi duniani zingehitajika fikra nyingi sana kuwezesha aya hizi kuelezea utendaji wa ulimwengu wetu. Lakini Dr. Bucaille alifanya hata na zaidi. Aligundua kwenye Kurani utabiri wa wanaanga:

> "Enyi jamii ya majini na watu! kama mtaweza kupenya katika mbingu na ardhi, basi penyeni! hamtapenya ila kwa nguvu!" (Surah 55:33).

Imedhaniwa zaidi kuwa Kurani inapozungumzia mbingu saba (k.m. Surah 78:122), namba saba ina maana tu ya wingi. Kutokana na hilo Dr. Bucaille anahitimisha kuwa Kurani inatamka wazi kuwa zitakuwako mbingu na dunia nyingi kwenye ulimwengu, ukweli ambao ungeweza kuthibitishwa tu kwenye wakati wetu (uk. 141). Hakika mtu anaweza kuhoji mantiki ya hoja kama hiyo.

Katika kutenda haki, itabidi mtu atambue pia kuwa Kurani ilishikilia mtazamo wa ulimwengu wa wakati ule, kuwa dunia ni kisahani na si tufe, kama tunavyojua leo:

> "Zul-qarnain (kulingana na mapokeo Alexander Mkuu)... alipoyafikia machweo ya jua alilikuta limetua kwenye chemchemi ya maji meusi" (Surah 18:83-86).

Bila ya kujaribu kusema zaidi ya andiko linayotaka kusema, tulinganishe hiyo na aya kutoka kwenye Biblia iliyoandikwa kama miaka 3500 iliyopita:

> [Mungu] *Hutandaza anga la kaskazini mahali patupu; naye huining'iniza dunia mahali pasipo na kitu*.
>
> (Ayubu 26:7)

Basi, hoja maarufu zaidi kwa madai ya kuwepokwa takwimu za kisayansi kwenye Kurani zisizoweza kujulikana wakati huo, ni elimuuzazi, au hasa taaluma ya maisha ya kiinitete, sayansi ya kutungwa kwa mimba na kukua kwa kiinitete cha

mwanadamu kwenye mji wa mimba wa mama yake. Makala mengi yenye ushawishi yanajaribu kuitafsiri Kurani ili maneno yake yamaanishe jambo ambalo hailisemi. Katika lugha ya madoido tunaarifiwa madaktari wamefadhaishwa na usahihi wa maelezo ya mfumo wa uzazi na utendaji wake. Hebu tuyaangalie haya:

"Tulikuumbeni kwa udongo, kisha kwa manii, kisha kuwa kipande cha damu, kisha huwa kipande cha nyama kinachoumbika na kisichoumbika; ili Tukubainishieni (kudra Yetu). Nasi Tunakukalisha matumboni Tunachokitaka mpaka muda uliowekwa, kisha Tunakutoeni kwa hali ya utoto" (Surah 22:5).

"Na kwa yakini Tulimuumba mwanadamu kwa udongo ulio safi. Kisha Tukamuumba kwa tone la manii lililowekwa katika makao yaliyohifadhika. Kisha Tukalifanya tone hilo kuwa pande la damu, na Tukalifanya pande la damu hilo kuwa pande la nyama, kisha Tukalifanya pande la nyama hilo kuwa mifupa, na mifupa Tukaivika nyama, kisha Tukamfanya kiumbe kingine. basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji!" (Surah 23:12-14).

"Yeye ndiye Aliyekuumbeni kwa udongo, kisha kwa pande la damu, halafu Akakutoeni katika hali ya mtoto" (Surah 40:67).

"(Mwanadamu) ameumbwa kwa maji ya kuchupa. Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na kifua (mbavu)" (Surah 86:6-7).

"Ambaye Ametengeneza umbo la kila kitu, na Akaanzisha umbo la mwanadamu kwa udongo. Na kisha Akakifanya kizazi chake kwa mchujo wa maji yaliyo madhalilifu" (Surah 32:7-8).

"Hukuumbeni matumboni mwa mama zenu - umbo baada ya umbo - katika viza vitatu" (Surah 39:6).



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 26 13-04-2022 12:22:09

> "Mwenyezi Mungu anajua kila abebacho mwanamke (katika mimba yake) na yanavyoviza matumbo yake na yanavyozidisha. na kila kitu Kwake kwa kipimo" (Surah 13:8).

Inapasa kutamkwa hapa kuwa vifungu vya hapo juu isipokuwa vile vilivyorudiwa (Surah 16:5, 80:19-20, 75:38-40, 18:38), vina *yote* inayosema Kurani kuhusu mada hii. Hatuoni dokezo la manii kurutubisha yai, bali tunayoona hasa ni dhana kuwa manii ndiyo mbegu iliyopandwa kwenye mji wa mimba ili ikomae. Katika kusahihisha jambo hili lililoachwa Dr. Bucaille ananukuu kwenye Hadith:

> "Alisema (huyo Nabii Mtakatifu): 'Kiini cha uzazi cha mwanaume ni cheupe na cha mwanamke ni cha manjano. Wanapokutana kimwili na kiini cha mwanaume kinazidi juu ya kiini cha mwanamke, anayeumbwa ni mtoto wa kiume kwa agizo la Mwenyezi Mungu. Kiini cha mwanamke kikizidi juu ya kiini kilichotolewa na mwanaume, anatengenezwa mtoto wa kike kwa agizo la Mwenyezi Mungu.' Wachache walisema: 'Ulichosema ni kweli, kweli wewe ni Mtume.' Kisha aligeuka akaenda zake. Mtume wa Mwenyezi Mungu (amani iwe juu yake) akasema: 'Aliniuliza kuhusu mambo kadha wa kadha ambayo sikuyajua hadi Mwenyezi Mungu aliponipa'" (Sahih Muslim Hadith 614).

Nadhani unafikiri kama mimi, hatuwezi kuyaona haya kuwa yanatia nuru. Na Hadith ifuatayo itahitaji sana kutafsiriwa ili ilete maana kwenye mawazo yetu ya karne ya 21:

> "Mtume wa kweli na aliyevuviwa kweli na Mwenyezi Mungu, alitusimulia: 'Kuumbwa kwa kila mmoja wenu huanza na mchakato wa kukusanya nyenzo kwa ajili ya mwili wake ndani ya siku arobaini mchana na usiku kwenye mji wa mimba wa mama yake. Kisha anakuwa bonge la damu nzito kwa muda kama huo (siku arobaini) na kisha anakuwa kama kipande cha nyama kwa kipindi kama



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 27 13-04-2022 12:22:09

> hicho. Kisha malaika hutumwa (na Mwenyezi Mungu) kwake na malaika huruhusiwa (huagizwa) aandike mambo manne: mahitaji yake, tarehe yake ya kufa, matendo yake, na kama atakuwa mkataliwa au mbarikiwa (baadaye) kisha uhai wake unapuliziwa ndani yake'" (Sahih Al-Bukhari Hadith 9.546, ona pia 4.430).

Itahitaji kitabu kizima kupitia kwa kina zaidi kwenye majadiliano haya, lakini machache niliyokuwa nayo yanaleta mwanga fulani kwenye hoja hii inayotawala. Kimsingi hoja nyingine zote ziko kwenye kiini kile kile. Kutokana na haya yote tunaweza kutoa uamuzi gani? Ni kawaida na inaeleweka kwa watu kuhoji kwa msingi wa mtazamo wao kuhusu ulimwengu. Wote tunaishi kwa kudhani kuwa mtazamo wetu kuhusu ulimwengu ni sahihi na wa kweli. Lakini lazima tujifunze kuhoji uhalali wa mawazo ya kila mtu yanayoamua matendo yake. Huu unaweza kuwa mchakato wa kutafakari na wakati mwingine kuhuzunisha sana.

Kama tunataka kuishi maisha ya kiroho yenye ukweli na maana, itabidi tuseme 'kwa heri' kwa maoni ya ummana tuitafute kweli ya Mungu. Bila ya kutaka kujiridhisha nafsi wala kutafuta ugomvi inabidi nikiri kuwa utafutaji wa asili ya kimungu ya Kitabu kwa namna tulivyoichunguza sasa hivi, huleta maswali mengi zaidi kuliko unavyoweza kutarajiwa kujibu.

Ninasikitika sana kuwa hasi kwa namna nyingi sana. Lazima uujue moyo wangu ili uifahamu nia inayoniongoza. Utajua kuwa si kupenda mabishano wala kujiridhisha nafsi kulikojificha. Ninachotamani ni kwamba tujikabidhi kwa Mungu kwa msingi wa taarifa za kweli kuhusu yeye. Barua hii inaweza kuchangia kidogo kwa sisi kufanya hivyo?

Wako wa kweli,

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 28 13-04-2022 12:22:09

## *Barua ya Sita*

# Mungu Yukoje?

*Mpendwa Abdallah*

Asante kwa maneno yako yanayovutia sana kwenye barua yako ya mwisho. Yote unayoandika ni ya kweli kupita kiasi. Ni rahisi kuondolewa kwenye masuala halisi - lakini wewe unaturudisha tena kwenye njia sahihi.

Unasema kuwa sote tunamzungumzia Mungu na tuna utambuzi fulani kuhusu Yeye. Hata hivyo tunapozungumza kuhusu Yeye, tunagundua kuwa utambuzi wetu unatofautiana, na pamoja na hayo mtazamo wetu kuhusu ulimwengu na mtindo wetu wa maisha. Kwa nini iwe hivyo huku wote tunatambua kuwa kuna Mungu mmoja tu? Tayari umelitoa jibu: Kwa sababu tunategemeza ufahamu wetu kuhusu Mungu kwenye vigezo vinavyotofautiana. Naona ninalazimika kujaribu kuelezea tunamaanisha nini - au bora zaidi, Nani - tunaposema 'Mungu'.

Mtu akiuchunguza utambuzi mwingi unaotofautiana kabisa ambao watu wanakuwa nao mara nyingi kuhusu Mungu, ataona kuwa wengi hufuata kitu kilichobuniwa na fikira zao. Itabidi tulifikirie hilo.

Mungu ni nani? Allah, kama anavyoonyeshwa na Uislamu, na Yahweh Elohim, kama anavyowasilishwa kwenye Biblia, ni yule yule? Kama jibu ni ndiyo, kwa nini tunapata taarifa zinazogongana kuhusu yeye? Nikushirikishe mtazamo wangu kuhusu hili.

Duniani kuna maelfu au hata mamilioni ya miungu wanaoheshimiwa au hata kuabudiwa, hata hivyo wewe na mimi tunaamini kuna Mungu mmoja, Mungu mmoja tu. Ninaamini pia kuwa tofauti zo zote zinazoelekea kuonekana kuhusu



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 29 13-04-2022 12:22:09

Mungu kwenye dini moja au nyingine haziakisi mgawanyiko ndani ya Mungu, bali ni matokeo ya taarifa za uongo au zisizo kamili kuhusu Yeye. Ninaamini kwa moyo wote kuwa kimsingi ni lazima ufahamu wote wa kweli kuhusu Mungu utoke kwa Mungu mwenyewe. Tunaweza kujua nini kuhusu Yeye?

Kwanza, napenda nitaje uumbaji. Ninazungumzia jumla ya vyote vilivyopo. Ulimwengu hutoa taarifa kuwa lazima kiwepo kitu kikubwa na chenye nguvu na akili zaidi kuliko tunavyoweza kutambua, ambacho ni mwandaaji wa vitu vyote.

Ninaamini kwa moyo wote kuwa kimsingi ni lazima ufahamu wote wa kweli kuhusu Mungu utoke kwa Mungu mwenyewe.

Hata hivyo uumbaji haufunui lo lote zaidi. Hauwezi kutuambia kama ustadi huu wenye nguvu ni nguvu tu ya namna fulani, au kama ina nafsi. Kwa hiyo naweza kusema salama kuwa ‘Mungu’ ni mweza wa yote na mwenye akili isiyo na mipaka, lakini nisingeweza kuhitimisha kwa uuchunguza ulimwengu kuwa Yeye ni nafsi, ni mtakatifu, mwenye haki, mwenye rehema au mwenye upendo. Wakristo na Waislamu hudai kwa haki anazo sifa hizi. Vitabu vyetu husema hivyo, na hata wanatheolojia wetu. Hata hivyo tunatofautiana katika utambuzi wetu wa asili ya Mungu.

Tuchukue neno haki. Ina maana kuwa Mungu ni mwema kabisa na kwa hiyo wakati wote atatenda haki? Kama Mungu ni mwema, anaweza kuumba uovu? Kama Yeye ni mwenye haki, anaweza kusababisha mtu atende dhambi,kisha amwadhibu mtu huyo kwa kufanya hivyo? Kama Mungu ni upendo, inawezekana hatayajali manufaa yetu ya milele? Kihisia wote tutajibu bila ya kusita kuwa Mungu hangeweza kuumba uovu au kumshawishi mtu atende dhambi, kisha amwadhibu kwa hilo, na kuwa hawezi kutelekeza viumbe wake. Utambuzi wetu wa asili kuhusu Mungu hutufanya tuone hivi. Tumshukuru Mungu, hapa tunachoamini mimi na wewe kihisia kinakubaliana kabisa na Biblia.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 30 13-04-2022 12:22:09

Lakini hili haliwezi kuzungumziwa kwenye Uislamu. Kulingana na Imam al-Barqavi (aliyekufa mwaka wa 1135 bK), mwanatheolojia na mchunguzi maarufu wa Kurani, Mwenyezi Mungu ni tofauti:

"Mwenyezi Mungu hapokei faida wala hasara kwa lo lote linaloweza kutokea. Makafiri wote wangekuwa waumini ... Hangepata faida. Kwa upande mwingine, waumini wote wangekuwa makafiri, Hangepata hasara. Anaweza kufanya Atakalo, na kila Anachotaka hutimia. Halazimishwi kutenda. Kila jambo, jema au ovu kwenye dunia hii, kipo kwa mapenzi Yake. Imani ya waumini na ucha Mungu wa washika dini ni mapenzi ya Mungu. Kama angebadilisha utashi Wake hangekuwako mwumini wa kweli wala mcha Mungu. Kutoamini kwa wasioamini ni utashi wake pia, hata ukafiri wa waovu, na bila ya utashi huo, hakungekuwako kutoamini wala kutokuwa na dini ... Yeye yuko huru kabisa kutaka na kufanya analopenda. Katika kuwaumba wasioamini, katika kuwataka wabaki katika hali hiyo; katika kuumba nyoka, nge na nguruwe; katika kutaka, kwa ufupi, yote yaliyo maovu. Mungu ana makusudio yenye hekima ambayo si lazima tuyajue."

('Haft sifat' kama ilivyonukuliwa kwenye Hughes 'Dictionary of Islam' uk.141).

Ni wazi kabisa kuwa anachotaka kuwasilisha al-Barqavi na wanatheolojia wengine walio wengi wa Kiislamu kwa miundo kama ulivyo huu, ni ukuu wa Mungu. Bila shaka msingi wa hili ni Kurani na Mapokeo, la sivyo hakuna ambaye angeikubali kauli kama hii:

> "Na Mwenyezi Mungu angalitaka, kwa yakini Angalikufanyieni kundi moja tu: Lakini Anamuachia kupotea Anayemtaka. Na Anamwongoa Anayemtaka. Na hakika mtaulizwa kwa yale mliyokuwa mkiyafanya." (Surah 16:93. Ona pia Surah 16:37; 6:149).



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 31 13-04-2022 12:22:09

Ninashindwa kuuona kuwa ni mfano wa haki na hukumu ya haki, mtu akihukumiwa kwa jambo alilolazimishwa na Mungu kulifanya.

Inaonekana kama vile ukuu wa Mwenyezi Mungu hubatilisha haki, huruma, na upendo. Hizi ni sifa ambazo hakika tunazitarajia kutoka kwa Mungu. Kwa kweli aya kama hizo, na ziko nyingi, hupingana na vifungu vingine vingi vya Kurani - pamoja na Shahada. Kwa kweli ninashindwa kuuona kuwa ni mfano wa haki na hukumu ya haki, mtu akihukumiwa kwa jambo alilolazimishwa na Mungu kulifanya. Hiki si kifungu kilichowekwa kando. Kinathibitishwa na aya kama zifuatazo:

"Atakaowaongoza Mwenyezi Mungu ndio watakaoongoka, na Atakaowaachia kupotea ndio watakaopata khasara. **Tumewaumbia Moto wa Jahannamu** wengi katika majini na **wanadamu**" (Surah 7:178, 79).

"Kama Tungalitaka hakika Tungeileta kila nafsi kwenye uwongozi wake wa kweli; lakini neno litokalo Kwangu litatimia, Nitaijaza jahanamu majini na wanadamu wote pamoja'" (Surah 32:130).

"**Allah huwapoteza anaowataka**, na huwaongoza anaowataka". (Surah 14:4, ona pia Surah 9:51, 5:20, 16:93, 37:96, 76:29-30, 4:88, 16:36, 6:149 na 7:158)

"Humsamehe Anayemtaka na Humwadhibu anayemtaka".

(Surah 5:20, soma pia Surah 37:96; 76:29 - 30; 4:88; 16:36; 6:149; 7:158)

Kauli kama hizo zinaungwa mkono sana na Hadith. Tuangalie tu vifungu viwili:

"Abu Huraira alitoa taarifa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (amani Iwe juu yake) amesema: **Mwenyezi Mungu alilithibitisha fungu lenyewe la uzinzi atakalojihusisha nalo mwanadamu. Hakutakuwa na kulikwepa**" (Sahih Muslim IV, uk. 1396 - 1398).



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 32 13-04-2022 12:22:09

> "Ya Abu Darda iliarifu kuwa Nabii Mtakatifu alisema: '**Allah alimwumba Adamu**, alipomwumba. **Kisha alimpiga** bega lake la kulia **akatoa jamii nyeupe** kama vile zilikuwa mbegu, na alimpiga bega lake la kulia **akatoa jamii nyeusi** kama vile yalikuwa makaa ya mawe. Kisha **aliwaambia wa bega lake la kulia: Nendeni Peponi na sijali. Akawaambia wa bega lake la kushoto: Nendeni Jehanamu na sijali'**" (Mishkat vol.3 p. 117).

Mtu yeyote mwenye rangi nyeusi akiamini hilo atatishwa kabisa na matarajio haya.

Al-Baqawi anaielezea kanuni iliyopelekea kwenye fundisho kama hilo:

> "Mwenyezi Mungu siyo tu anaweza kufanya jambo lo lote, Yeye ndiye pekee hasa anayefanya jambo lo lote. Mwanadamu anapoandika, ni Mwenyezi Mungu aliyeumba kwenye akili zake utashi wa kuandika. Wakati huo huo Mwenyezi Mungu huutoa uwezo wa kuandika, kisha huuleta msukumo wa mkono na wa kalamu na mwonekano kwenye karatasi. Mambo mengine yote ni baridi, Mwenyezi Mungu pekee ndiye mtendaji."

Swali linalojitokeza ni: hapa upendo wa Mungu uko wapi - na rehema na neema Yake, ambapo wote tunategemea? Ninafikiria tena kutokamilika na kutokuwa safi kwetu. Ukijitahidi ukalichanganua hili kwenye Kurani, utaona kuwa Mwenyezi Mungu anawapenda tu wenye haki na wema. Na sisi je, tuliokosa tukakiuka maagizo ya Mungu? Alichowahi kuandika al-Ghazzali kinatisha na sihitaji kumtambulisha kwako:

> "Upendo ni kuhisi hitaji la mpendwa, na kwa kuwa Allah hawezi kusemekana kuwa ana haja au uzoefu wa hitaji, haiwezekani Mwenyezi Mungu kupenda."

Mtazamo kama huo kuhusu Mungu ni kinyume kabisa na Biblia. Kama vile kauli ya msingi kuhusu Mungu kwenye



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 33 13-04-2022 12:22:09

Uislamu ni Allahu-akbar, vivyo hivyo Biblia hutoa kauli kuwa "Mungu ni Pendo". Ndiyo, Yeye ni mtakatifu na mwenye haki katika hukumu zake. Tunatambua kuwa ufahamu huu wenyewe unatisha sana kwetu, kwa sababu sisi si wenye haki. Lakini haki ya Mungu imefunganishwa na huruma yake na upendo wake. Angalia Biblia inavyofundisha:

Kama vile kauli ya msingi kuhusu Mungu
kwenye Uislamu ni Allahu-akbar,
vivyo hivyo Biblia hutoa kauli
kuwa "Mungu ni Pendo."

Kuhusu ukuu Wake:

*"Hili ndilo alilonena Bwana wakati aliposema: " 'Miongoni mwa wale watakaonikaribia nitajionyesha kuwa mtakatifu; machoni pa watu wote nitaheshimiwa.' "* (Walawi 10:3)

*Mtukuzeni Bwana Mungu wetu, na mkaabudu katika mahali pa kuwekea miguu yake; yeye ni mtakatifu.*

(Zaburi 99:5)

*"Ninaishi mimi mahali palipoinuka na patakatifu."*

(Isaya 57:15)

*Yeye peke yake ambaye hapatikani na mauti, na anakaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ambaye hakuna mwanadamu aliyemwona wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye milele. Amen.* (1 Tim 6:16)

*"Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako, aliyeko na atakayekuja."*

(Ufunuo 4:8)

Kuhusu anachotarajia Mungu kwetu:

*Bwana Mungu wako anataka nini kwako ila kumcha Bwana Mungu wako, kwenda katika njia zake, kumpenda*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 34 13-04-2022 12:22:09

*na kumtumikia BWANA Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, na kuyashika maagizo ya BWANA na amri zake ninazokupa leo kwa mafanikio yako mwenyewe?*
(Kumbukumbu 10:12-13)

Kuhusu mtazamo wa Mungu kwa wanadamu:

*Wamenipa visogo vyao wala hawakunigeuzia nyuso zao; lakini wakiwa katika taabu, wanasema, 'Njoo utuokoe!'*
(Yeremia 2:27)

Kuhusu juhudi za Mungu za kutuleta Kwake:

*Laiti ungesikiliza kwa makini maagizo yangu, amani yako ingekuwa kama mto, haki yako kama mawimbi ya bahari.*
(Isaya 48:18)

*... kwa kuwa mimi ni mwenye huruma,' asema Bwana, 'Sitashika hasira yangu milele. Ungama dhambi zako tu: kwamba umemwasi BWANA Mungu wako, ... nawe hukunitii mimi,' asema Bwana.* (Yeremia 3:12 - 13)

*Tegeni sikio mje kwangu, nisikieni mimi, ili nafsi zenu zipate kuishi. Nitafanya agano la milele nanyi.* (Isaya 55:3)

*"Nimeyafuta makosa yako kama wingu, dhambi zako kama ukungu wa asubuhi. Nirudie mimi, kwa kuwa nimekukomboa wewe."* (Isaya 44:22)

*Huchunga kundi lake kama mchungaji wa mifugo: Hukusanya wana-kondoo katika mikono yake na kuwachukua karibu na moyo wake, huwaongoza taratibu wale wanyonyeshao.* (Isaya 40:11)

*'Kwa kuwa hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo: Mimi mwenyewe nitawaulizia kondoo wangu na kuwatafuta. ... Mimi mwenyewe nitawachunga kondoo zangu na kuwafanya wapumzike,' asema Bwana Mwenyezi.*
(Ezekieli 34:11, 15)

Miaka 600 baadaye Yesu alisema:

*Ndipo Yesu akawaambia mfano huu: "Ikiwa mmoja wenu ana kondoo mia moja, naye akapoteza mmoja wao, je, hawaachi wale tisini na tisa nyikani na kwenda kumtafuta huyo aliyepotea mpaka ampate? Naye akishampata, humbeba mabegani mwake kwa furaha.* (Luka 15:3-5)

*"Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo ... Mimi ndimi mchungaji mwema. Ninawajua kondoo wangu nao kondoo wangu wananijua. ... Baba yangu ananipenda kwa sababu ninautoa uhai wangu ili niupate tena ... Kondoo wangu huisikia sauti yangu nami nawajua, nao hunifuata, nami ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka katika mikono yangu."* (Yohana 10:11-17, 27-28)

Utakuwa umetambua kuwa maandishi yangu si ya fundisho la kitheolojia kuhusu Mungu. Lakini utakuwa umepata 'hali' fulani kutoka kwenye moyo wa Mungu. Na utakuwa umeigundua pia tofauti halisi kati ya mitazamo yetu kuhusu Mungu, na huenda pia unaanza kuelewa au hata kuikubali shauku yangu kwa ajili yake. Ni wazi kwamba kwenye barua kama hii naweza kugusia tu vipengele vidogo vya asili ya Mungu, tena kwa ufupi sana.

Ninapofunga naomba nijaribu kueleza kwa maneno machache kiini cha utambuzi wetu unaotofautiana kuhusu Mungu:

Katika juhudi ya kumheshimu Mungu, wewe kama Mwislamu hukazia kwenye uweza na nguvu zake. Uislamu hudai kunyenyekea chini ya utawala wa Mungu, na wewe hujaribu kuwajibika kwa kutii sheria zake nyingi. Lakini kutokana na mtazamo wako juu ya Mungu huwezi kuwa na hakikisho lo lote kuhusu hali yako mbele ya Mungu - hadi Siku ya Hukumu.

Huku Uislamu ukishikilia kuwa Mungu yuko *tansih*, (mbali katika utukufu wake wenye fahari, na amejitenga na mengine

yote), Biblia humwonyesha Mungu kama anayekubali yaliyo ya chini, ambaye upendo wake na huruma yake kwa mwanadamu hutengeneza njia ya kumkomboa.

Kutoka kwenye Biblia ninajua kuwa Mungu ni mtakatifu, na ninajua kuwa mimi si mtakatifu. Ninajua pia kuwa Mungu ana haki ya **kudai** haki kutoka kwetu, lakini **anatupa** sisi haki yake mwenyewe. Katika upendo wake anajitoa yeye mwenyewe kwa ajili yetu. Katika Yesu yeye ndiye 'mchungaji mwema' wetu, anayemtafuta kondoo aliyepotea hadi ampate, kisha huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo wake. Hili huakisi hasa upendo wa Mungu kwa ajili yetu, na upendo huo huonyesha thamani anayompa kila mmoja wetu. Sisi si kama panya au chawa machoni kwake. Tukiupokea mkono wake aliotunyoshea, sisi ni watoto wake wapendwa!

Kizuizi kwa Mungu si dhambi yetu,
maana upendo wake tayari umeishinda,
bali ni sisi kutokuwa tayari
kuipokea karama Yake ya upendo,
msamaha kwa njia ya Yesu.

Hata hivyo kuna sharti moja. Mara tu kabla ya kifo chake msalabani, Yesu akiwa katika huzuni alitamka maneno haya yanayovunja moyo akiwaambia waliompinga:

> *"Mara ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako pamoja, kama vile kuku akusanyavyo vifaranga wake chini ya mabawa yake, **lakini** hukutaka!"* (Mathayo 23:37)

Kizuizi kwa Mungu si dhambi yetu, maana upendo wake tayari umeishinda, bali ni sisi kutokuwa tayari kuipokea karama Yake ya upendo, msamaha kwa njia ya Yesu.

Siyo kweli inavyosema methali kwamba "kinywa cha mtu huyanena yale yaliyoujaza moyo wake?" Ni jinsi ilivyo kwangu



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 37 13-04-2022 12:22:09

ninapoandika kuhusu Mungu. (Pia asili ya methali hiyo ni kwenye Biblia katika Mathayo 12:34.)

Lakini sasa lazima niombe radhi kwa urefu wa barua hii! Hata hivyo utakubali kuwa inafaa kwa mada tuliyoigusia.

Salamu zenye upendo!

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 38 13-04-2022 12:22:09

### *Barua ya Saba*

## Neno Rahisi tu: Dhambi

*Mpendwa Abdallah*

Ninathamini jinsi unavyofurahia mada za msingi za imani yetu. Baada ya kutumia muda tukiichunguza mada yenyewe ya Mungu ni nani, ninapendekeza tuangalie mada yenye tatizo linalotuathiri kila siku, na kwa sababu hiyo ni muhimu zaidi. zaidi. Ni ile dhana ya dhambi.

Muda fulani uliopita Mwislamu tunayefahamiana aliniuliza kwa nini Wakristo, kama alivyoliweka, 'wameshikiliwa na dhambi' kiasi hicho. Nilimjibu, "Kwa sababu dhambi ndiyo inayotufanya kuwa kinyume na Mungu na kutuathiri kila siku ya maisha yetu". Kwa kawaida sisi sote tunataka tuishi bila dhambi, hata hivyo wakati wote tunaizalia matunda. Kama tunataka kuishi na Mungu, hii ni mada husika. Inaelezea moja la masuala ambalo huenda ni muhimu zaidi katika maisha. Mtu ye yote aliye mwaminifu na mwenye dhamiri inayotenda kazi na utambuzi wa msingi wa maadili, atashitushwa na utayari wetu wa kufikiria au kufanya tunayojua kuwa si sahihi. Hata mababa wa kwenye Biblia waligandamizwa na mlemeo wa jambo hili.

Adamu alimwasi Mungu. Kaini alimwua ndugu yake Habili. Nuhu alilewa hadi akapagawa, mabinti wa Lutu walilala na baba yao, Ibrahimu alisema uongo kuwa mke wake ni dada yake, Yakobo alikuwa mdanganyaji, Musa alikuwa mwuaji na alitenda kinyume na maagizo ya Mungu, Daudi alizini na kupanga mauaji, na inaendelea.

Kwa nini sote tuna mwelekeo huu wa kutenda dhambi, hata kinyume na utashi wetu? Ni dhahiri kuwa huu ni urithi wa asili yetu kutoka kwa wazazi wetu na mababa zetu. Tayari wakati wa Nuhu:

*BWANA akasikitika ... moyo wa Mungu ukajaa masikitiko.*
(Mwanzo 6:6)

*BWANA akaona jinsi uovu wa mwanadamu ulivyokuwa mkubwa duniani, na ya kuwa kila mwelekeo wa mawazo ya moyo wake wakati wote ulikuwa mbaya tu.*
(Mwanzo 6:5)

Hapo mwanzo Adamu alipoumbwa, Mungu alimpa kuchagua kutenda kwa kumkubalia au kwa kumpinga. Bila ya uchaguzi huo mwanadamu angekuwa kama roboti. Hangewajibishwa. Hangeweza kumpenda Mungu na mwanadamu mwenzake. Uwezo wa kuchagua ni jambo la msingi.

Kukosea ni kukosea tu, haina tofauti kama ni kwa kiwango kidogo sana au kikubwa sana.

Tunasoma kuwa Adamu na Hawa waliamua kupinga kusudi la Mungu. Tangu wakati huo kila mwanadamu amefanya maamuzi mabaya. Adamu, pamoja na wote walioishi tangu wakati huo, wamehoji tena na tena makusudio mazuri ya Mungu na wamejaribu kuwa 'mungu' wa maisha yao wenyewe. Lakini ni Shetani mdanganyaji anayekuwa huyo 'mungu'. Ndiyo sababu hatuwezi kuacha kutaka kufanya dhambi.

Agano Jipya linasema jambo ambalo tutakubali sote:

*Sielewi nitendalo, kwa maana lile ninalotaka kulitenda, silitendi, lakini ninatenda lile ninalolichukia ... ninafahamu kwamba hakuna jema lolote likaalo ndani yangu, yaani, katika asili yangu ya dhambi. Kwa kuwa nina shauku ya kutenda lililo jema, lakini siwezi kulitenda.*
(Warumi 7:15-18)

Ni kweli tuko vile? Kwa nini tunashindwa? Ili kujibu swali letu kwa usahihi, inabidi tufafanue maana ya neno 'dhambi'.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 40 13-04-2022 12:22:09

Maana halisi ya neno lililotafsiriwa kama 'dhambi' katika Kiebrania na Kigiriki (lugha ambamo Biblia iliandikwa hapo mwanzo) ni 'kukosea lengo au kusudi'. Mpiganaji huchukua upinde na mshale, hulenga na kupiga. Lakini mshale hukosa! Kusudi halijatimizwa. Haijalishi kama amekosea kiasi kidogo sana, au kikubwa sana. Hata nia yake njema ya kupiga hatimaye halina matokeo. Maana nyingine za neno hilo ni 'kuondoka kwenye njia iliyowekwa, kuasi mamlaka halali, kukiuka sheria ya Mungu, kuvunja agano, kukosa uaminifu, uhaini na ubatili' - yote kuhusiana na Mungu. Mzizi wake ni 'chaguo dhahiri au upendeleo wa msingi kwenye ubinafsi badala ya Mungu' (A.H. Strong).

Kanuni inayotawala mwelekeo wetu wa kufanya makosa imeelezwa kwenye Agano Jipya:

> *Kwa maana mwili hutamani yale yaliyo kinyume na Roho, naye Roho hutamani yale yaliyo kinyume na mwili. Roho na mwili hupingana na kwa sababu hiyo hamwezi kufanya mnayotaka.* (Wagalatia 5:17)

Nina hakika tunakubaliana kuwa kutokana ukweli kwamba Mungu alituumba naye ndiye Bwana, ndiye Bwana, ana haki ya kutarajia kuwa tutafikiri na kufanya kulingana na mapenzi na makusudio yake. Ili atuadibishe kuhusu hili, ametupa Neno lake, linalotuambia kuhusu kupingana kati ya wema na uovu, sahihi na kosa, na jinsi ya kuushinda uovu. Anatuambia pia kuhusu mapenzi yake kwa ajili yetu:

> *Mapenzi ya Mungu ni kwamba ninyi mtakaswe.*
> (1 Wathesalonike 4:3)

na

> *Mkajivike utu mpya, ulioumbwa sawasawa na mfano wa Mungu katika haki yote na utakatifu.* (Waefeso 4:24)

Utakatifu ni neno la kibiblia lenye maana ya kutengwa kwa ajili ya kusudi la Mungu. Bila shaka maana hii mara nyingi



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 41 13-04-2022 12:22:09

sana hugongana na matamanio yetu binafsi, yanayotafuta kujiridhisha wenyewe. Inawezekana tunajitahidi kumheshimu na kumpendeza Mungu, lakini matakwa ya ubinafsi wetu wakati wote yanakuwa na nguvu zaidi.

Tupende tusipende, ndani kabisa ya kila mmoja wetu kuna msukumo wa kutenda dhambi usioweza kuzuilika.

Tuna mwelekeo wa kujilinganisha na watu wengine, na hilo linaweza kuridhisha kwa kiasi fulani. Lakini Mungu hutuhukumu sisi kwa kiwango chake mwenyewe cha kimungu. Watu wengi sana wanafundishwa kimakosa kuwa ikiwa asilimia 51 ya yale wanayofanya yanakubaliana na sheria za Mungu, basi itatosha kuwapeleka paradiso au mbinguni. Lakini anachotaka Mungu ni moyo wetu wote:

*Kwa maana mtu yeyote anayeishika sheria yote lakini akajikwaa katika kipengele kimoja tu, ana hatia ya kuivunja sheria yote.* (Yakobo 2:10)

Aya hii hutufunulia hali isiyo na tumaini ambamo tunajikuta. Lazima tuelewe kweli fulani ya msingi: **Sisi si wenye dhambi kwa sababu tumetenda dhambi. Bali tunatenda dhambi kwa sababu sisi ni wenye dhambi!**

Dhambi huja kama jambo la kawaida. Imo kwenye asili yetu. Hatuhitaji mafunzo kuitenda. Tupende tusipende, ndani kabisa ya kila mmoja wetu kuna msukumo wa kutenda dhambi usioweza kuzuilika. Dhambi ni yote yaliyo kinyume na asili ya Mungu. Huanza na kukosa wema na kushindwa kupenda, hali inayogeuka na kuwa chuki, matengano, wivu, kusengenya, husuda, uchoyo, hasira na tamaa, bila ya kuzitaja dhambi mbaya zaidi. Lakini ndani ya mioyo yetu bado tunataka tuwe safi.

Inagusa moyo kusoma Zaburi ya Daudi aliyepondeka moyo,



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 42 13-04-2022 12:22:09

ambayo aliiomba baada ya kufanya uzinzi. Alisihi jambo moja tu:

> *Unioshe na uovu wangu wote na unitakase dhambi yangu ... Dhidi yako, wewe peke yako, nimetenda dhambi na kufanya yaliyo mabaya machoni pako ... Ufiche uso wako usizitazame dhambi zangu, na uufute uovu wangu wote. Ee Mungu, uniumbie moyo safi ...* (Zaburi 51:2, 4, 9-10)

Daudi alitambua kuwa hakuwa amewakosea tu watu, bali hasa alikuwa amemkosea Mungu aliye mtakatifu!

Ninaona tukomee kwenye jambo hili. Hapo kuna mengi sana ya kufikiria. Napenda niendelee na kuhitimisha somo hili kwenye barua yangu inayofuata. Ikiwa uliiona barua hii kuwa ni hasi mno, uko sahihi kabisa. Itafadhaisha sana kukomea hapa bila tumaini la ufumbuzi. Tumshukuru Mungu, anatoa ufumbuzi.

Hivyo basi, as-Salam'allay-kum!

Wako wa kweli,

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 43 13-04-2022 12:22:10

*Barua ya Nane*

## Ilwapo tutapata kile tunachostahili

*Mpendwa Abdallah*

Asante sana kwa juhudi yako ya kunijibu kwa namna iliyo kamili na yenye kuelewa! Mara nyingi watu huelekea kuona kuwa kuna dhambi kubwa na ndogo: dhambi zinazoweza kufidiwa kwa 'matendo mema', zinazohitaji toba na zisizoweza kusamehewa. Biblia ina ukadiriaji ulio tofauti.

Huenda jambo linaeleweka vizuri zaidi ukiangalia kile ambacho Yesu alikiita 'Amri Kuu'. Huo kweli ndio ujumuishaji wa Sheria ya Mungu, zile Amri Kumi:

> *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote ... Mpende jirani yako kama nafsi yako."* (Mathayo 22:37, 39)

Hii ndiyo nia ya Mungu kwetu. Kupungua lo lote katika hayo ni 'kulikosa lengo' alilo nalo Mungu kwa ajili yetu. Utaikumbuka istiari hii kutoka kwenye barua yangu ya mwisho.

Kufanya mapenzi ya nafsi au kujiridhisha badala ya kufanya mapenzi ya Mungu, siyo tu kulikosa lengo, lakini pia kuna matokeo yake. Biblia inasema tu kuwa:

> *... maovu yenu yamewatenganisha ninyi na Mungu wenu.* (Isaya 59:2)

Dhambi ni namna fulani ya 'kadi nyekundu', kama kwenye mashindano ya mpira wa miguu. Ina maana: "Uko nje!" Dini huwataka wafuasi wake wawe na juhudi ya kutenda kwa usahihi, na dhambi ikitendeka, wajaribu kuifidia kwa 'matendo mema'. Hili hutufanya tujisikie vizuri. "Ninaweza!" Ni asili yetu kujaribu kumtuliza Mungu kwa kutoa fidia kwa dhambi yetu. Hatimaye ttunadhani kwamba ilimradi hatufanyi shirk



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 44 13-04-2022 12:22:10

au kufr, hatuna tatizo kwa Mungu. Hili ni sawa na mkosaji aliyehukumiwa kutarajia kuachiwa huru akiahidi tu kufanya ‘tendo jema’ la kufidia kosa lake, na akiongezea ahadi kuwa hatarudia kosa lile. Haki ya Mungu haifanyi kazi kwa namna hiyo wala haiiakisi rehema na neema yake. Mungu asipoiondoa, dhambi humtenganisha mkosaji atoke kwake milele!

Kupungua lo lote katika hayo ni
‘kulikosa lengo’ alilo nalo Mungu
kwa ajili yetu.

Kitabu cha mwisho kwenye Biblia kina maono juu ya matokeo yenye uteketevu ya kupungua hivyo:

> *Nami nikawaona wafu wakubwa na wadogo, wakiwa wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi na vitabu vikafunguliwa. ... Hao wafu wakahukumiwa sawasawa na matendo yao kama yalivyoandikwa ndani ya hivyo vitabu.*
> (Ufunuo 20:12)

Siku ya Hukumu ni siku ya kuvuna. Kila mtu atapokea alichopanda, ndicho anachostahili. Ni kutekelezwa kwa hukumu ya Mungu.

Hakimu atakuwa Yesu, kama yeye mwenyewe alivyotamka:

> *“Mwana wa Adamu* [yaani Yesu] *atakapokuja katika utukufu wake na malaika wote watakatifu pamoja naye, ndipo atakapoketi juu ya kiti cha enzi cha utukufu wake. Mataifa yote watakusanyika mbele zake, naye atawatenga kama mchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi. Atawaweka kondoo upande wake wa kuume na mbuzi upande wake wa kushoto. Ndipo Mfalme atawaambia wale walioko upande wake wa kuume, ‘Njoni, ninyi mlioarikiwa na Baba yangu, urithini Ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuumbwa kwa ulimwengu.’ ... Kisha atawaambia wale walio upande wake wa kushoto, ‘Ondokeni kwangu,*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 45 13-04-2022 12:22:10

*ninyi mliolaaniwa, nendeni kwenye moto wa milele, ulioandaliwa kwa ajili ya Ibilisi na malaika zake'. ... Ndipo hawa watakapoingia kwenye adhabu ya milele, lakini wale wenye haki wataingia katika uzima wa milele.*

(Mathayo 25:31-34, 41, 46)

Siku ya Hukumu ni siku ya kuvuna.
Kila mtu atapokea alichopanda,
ndicho anachostahili.

*Mliobarikiwa na Baba yangu*, yangu, wanaourithi Ufalme wa Mungu, hao ni nani? Hawa ni watu wasio na dhambi? Tukikiangalia kifungu kwa makini tutaona kuwa si wale wanaostahili kuwa kwenye uwepo wa Mungu, bali ni wale wanaorithi. Hilo tutalielewa vipi? Warithi wa mtu ni watoto wake. Hii ni kawaida. Hawairithi bahati yao kwa sababu wanaistahili, bali kwa sababu hao ni watoto wa mtoa wosia. Urithi hupatikana akiisha kufa mtoa wosia. Katika Agano lake Jipya Mungu anatumia mfano ule. Kila mtu anayepokea msamaha kwa njia ya Yesu huwa jamii ya Mungu, maana kizuizi kilichotutenganisha na Mungu kimeondolewa, tumekuwa watoto wa Mungu, na tunaweza kwa furaha kumwita Mungu Baba yetu! Lakini ili awe 'wa nyumbani kwa Mungu' lazima mtu azaliwe humo. Imeandikwa kuhusu Yesu:

*Alikuja kwa walio wake, lakini wao hawakumpokea.* [jina Yesu lina maana ya Mwokozi] *... aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake. Hawa ndio wasiozaliwa kwa damu, wala kwa mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu.* (Yohana 1:11-13)

Akilifafanua hili Yesu alisema:

*"Amin, amin nakuambia, hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa mara ya pili." ...*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 46 13-04-2022 12:22:10

*"Amin, amin nakuambia, hakuna mtu yeyote anayeweza kuingia Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa kwa maji na kwa Roho. Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho. Kwa hiyo usishangae ninapokuambia huna budi 'kuzaliwa mara ya pili.'"* (Yohana 3:3-7)

Mtu anahitaji kuifikiri vizuri ili aielewe maana ya ndani zaidi ya sitiari hii. Wote tuko hai, kwa sababu tulizaliwa katika ulimwengu huu. Huko kulikuwa kuzaliwa miili yetu. Yesu alisema ili kuwa mtu wa kweli kama Mungu alivyokusudia, lazima pia azaliwe kiroho. Bila ya kuzaliwa kiroho mtu huwa amekufa kiroho.

... si wale wanaostahili kuwa
kwenye uwepo wa Mungu,
bali ni wale wanaorithi.

Kuzaliwa kiroho ukawa 'familia' ya Mungu hufanikiwa kwa njia ya imani katika Yesu. Imani hii siyo tu inayasadiki aliyoyafanya kwa ajili yetu, bali pia inalitambua hitaji letu la msamaha wake. Ni yeye aliyeuawa badala yetu. Tukizaliwa upya tunakuwa watoto wa Mungu, na tunakuwa warithi wake. (Warumi 8:17, Wagalatia 3:29)

Tukilielewa hili tutaikubali kauli iliyomo kwenye Agano Jipya:

*Lakini Mungu kwa upendo wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, 5hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu ... Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala si kwa matendo yenu mema. ... ili mtu yeyote asije akajisifu.* (Waefeso 2:4- 5, 8, 9)

Kwa sababu wote tumefanya dhambi, wote tunaitegemea kabisa huruma ya Mungu.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 47 13-04-2022 12:22:10

> Lakini ili awe ‘wa nyumbani kwa Mungu’,
> lazima mtu azaliwe humo.

Ikiwa hali ni hiyo, huleta hoja kama kweli jitihada yetu ya kuishi kwa haki ni ya lazima. Si kama njia ya kuacha dhambi za zamani au kustahili! Mungu anataka watoto wake ‘wakue’ kiroho kwa kubadilishwa zaidi na zaidi wakiakisi Yeye alivyo! Yesu aliwahi kusema:

*“Kwa hiyo kuweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.”* (Mathayo 5:48)

Lakini hata tukijaribu kiasi gani, asili yetu ya kale haikubaliani. Maadamu tukiwa katika maisha haya, hatuwezi kuwa wenye haki machoni pa Mungu kwa juhudi zetu wenyewe. Wala sheria ya Mungu haiwezi kutuhesabia haki wala kutusamehe. Sheria huamua tu ni lipi jema na ni lipi baya:

*Kwa hiyo hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria.*
(Warumi 3:20)

Ndiyo sababu Mungu kwa rehema yake anatupa haki yake yeye mwenyewe. Likizungumzia Wayahudi waliojaribu kwa juhudi yao wenyewe kuishika sheria, Agano Jipya linasema:

*Kwa maana ninaweza nikashuhudia wazi kwamba wao wana juhudi kubwa kwa ajili ya Mungu, lakini juhudi yao haina maarifa. Kwa kuwa hawakuijua haki itokayo kwa Mungu, wakatafuta kuweka haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu.* (Warumi 10:2, 3)

Hii kamwe haikuwa tofauti, maana tayari tulisoma kuhusu Ibrahimu kuwa:

*... akamwamini Bwana, naye kwake hili likahesabiwa kuwa haki.* (Mwanzo 15:6)

Sasa sijui wewe kama Mwislamu utaijibuje hii ambayo



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 48 13-04-2022 12:22:10

huenda kwako ni ‘lugha’ ngeni kabisa. Inakuambia - kama inavyofanya kwa Wayahudi - kuwa kwa kujaribu kuanzisha staha au haki mbele za Mungu, kwa kweli mtu hajitiishi kwa Mungu kama atakavyo!

Msingi wa imani yetu katika Mungu ni kuwa hatuwezi kufanya jambo lo lote kuupata uzima wa milele, lakini tunategemea ukombozi (wokovu) wake. Tayari tuliona kuwa wokovu hutolewa na Mwokozi. Huyo ni Yesu. Wokovu ni kusamehewa. Kwa kweli tulichopewa ni zaidi ya msamaha. Hasa Mungu anasema:

> *“... nitasamehe uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena.”* (Yeremia 31:34)

> *Utatuhurumia tena, ... na kutupa maovu yetu yote katika vilindi vya bahari.* (Mika 7:19)

> *Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo Mungu alivyoziweka dhambi zetu mbali nasi.* (Zaburi 103:12)

Siyo tu kwamba Mungu hutusamehe na kuturidhia, bali hasa huahidi kuzisahau dhambi zetu. Hutufanya tuwe safi kama vile kamwe hatukuwahi kutenda dhambi. Kumbukumbu zetu huko mbinguni ni safi. Majina yetu yameandikwa kwenye ‘Kitabu cha Uzima’ (ona pia Danieli 12:1; Wafilipi 4:3; Ufunuo 20:12, 15; 21:27). Hii ndiyo hali ya uamuzi inayoamua kuingia kwetu kwenye utukufu wa Mungu wa milele. Kwa ufupi, tumepatanishwa na Mungu na tuna amani na Yeye:

> *Haya yote yanatokana na Mungu, ambaye ametupatanisha sisi na nafsi yake kwa njia ya Yesu Kristo.*
> (2 Wakorintho 5:18)

Sasa utaelewa kwa nini sisi Wakristo tunamtegemea sana Yesu. Ndiye nafasi yetu pekee. Yesu mwenyewe alisema:

> *“Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu.”* (Yohana 14:6)

Mwisho, lakini si kwa ubora, nataka nitaje swali nililoulizwa



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 49 13-04-2022 12:22:10

mara nyingi: Mbona watu wajaribu kufanya matendo mema, ikiwa kwa vyo vyote vile dhambi zao zitasamehewa? Sawa, tunataka tumpendeze Baba yetu! Ni kutokana na shukrani maana ametuokoa! Upendo wetu kwa Mungu hutufanya tuchukie dhambi, kwa sababu Yeye anaichukia na inamwumiza.

Sasa utaelewa kwa nini sisi
Wakristo tunamtegemea sana
Yesu.Ndiye nafasi yetu pekee.

Biblia humwasilisha Mungu kama anayeathiriwa na kuhuzunishwa na dhambi yetu, na kwa sababu tunamtumikia na tunampenda, tunajitahidi tuwe kama anavyotaka tuwe. Ruhusu vifungu vichache vilionyeshe hili:

*... mambo yote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo na sifa njema, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote ya kupendeza, yoyote yenye staha, ukiwepo uzuri wowote, pakiwepo chochote kinachostahili kusifiwa, tafakarini mambo hayo.* (Wafilipi 4:8)

*... msiwe na lawama wala hatia, bali mwe wana wa Mungu wasio na kasoro katika kizazi chenye ukaidi na kilichopotoka, ambacho ndani yake ninyi mnang'aa kama mianga.* (Wafilipi 2:15)

Na kwa nini tunajaribu kuishi vema? Kwa sababu:

*... upendo wa Kristo unatutia nguvu.* (2 Wakorintho 5:14)

Sasa unataka kuniuliza, wako wapi hao Wakristo walio tayari kuishi hivi? Unawapata katika kila nchi na kila jamii, kwenye baadhi ya nchi wengi zaidi - katika nyingine wachache. Idadi zao si kubwa na mara nyingi hawajulikani. Lakini ukiwatafuta, utawapata. Lakini tafadhali utambue tena, si wakamilifu. Ukamilifu hauwezi kuonekana duniani. Lakini watakuwa na utayari ambao umeshatajwa kwenye Biblia:



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 50 13-04-2022 12:22:10

*"Si kwamba nimekwisha kufikia . . . lakini ninafanya jambo moja: Ninasahau mambo yale yaliyopita, nakaza mwendo kufikia yale yaliyo mbele. Nakaza mwendo nifikie ile alama ... ya mwito mkuu wa Mungu ambao nimeitiwa ...*

(Wafilipi 3:12-14)

Pamoja na salamu za kweli, ni mimi

Wako wa kweli,

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 51 13-04-2022 12:22:10

*Barua ya Tisa*

## Kwa jinsi gani Yesu ni wa pekee?

*Mpendwa Abdallah*

Nilijua utatoa hoja kwenye barua yangu iliyopita - na ndivyo ulivyofanya. Ulinukuu Surah 4:171 kutoka kwenye Kurani: "Isa hakuwa zaidi ya nabii." Inaeleweka kuwa unataka ukae kwenye eneo ulilozoea, maana linaonekana kama ni salama. Naomba nikuchukulie kwenye hilo kwa kukuomba uusome muktadha wa nukuu yako na huenda vifungu vingine vichache kutoka kwenye Kurani - kisha ukiangalie tena ulichoandika? Tunasoma kuhusu Isa kuwa:

- **Alikuwa Masihi** (Sura 4:171) (Biblia: Yohana 1:41, 4:25, 26). Angalizo: Kurani haifafanui neno la 'Masihi'. Kulingana na ufahamu wa Kiyahudi na Kikristo Masihi aliyetarajiwa alikuwa atumwe na Mungu kuwakomboa watu kutoka kwenye kifungo cha dhambi.
- **Alikuwa Roho itokayo kwa Mungu** (Sura 4:171).
- **Alikuwa Neno la Mungu** (Sura 4:171) (Biblia: Yohana 1:1-14). Tunaona kuwa Neno la Mungu ni Wazo la Mungu na pamoja na hilo, sehemu ya Mungu!
- **Aliumba uhai na kuponya wagonjwa** (Sura 3:49), (Biblia: Mathayo 11: 1-6).
- **Ni Ishara kwa wanadamu na Rehema ya Mungu** (Sura 19:21) (Biblia: Luka 2:25-32).
- **Ni Mwenye heshima katika dunia na Akhera** (Sura 3:45) (Biblia: Waebrania 1-3; Wakolosai 1:16, 2:9).
- **Alichukuliwa na Mungu hadi mbinguni** (Sura 4:158) (Biblia: Matendo 1:9-11).

- **Atarudi duniani kwa ajili ya hukumu** (Sura 43:61, Mishkat IV. Kurasa 78 - 80) (Biblia: Yohana 14:1-6; 5:22, 25-27).
- **Alikuwa mtakatifu** (Sura 19:19) (Biblia: Waebrania 7:26).

Tayari tuliona kuhusiana na habari hiyo kuwa kinyume na imani iliyoenea kwa umma, Biblia na Kurani havikubali kuwa manabii wote hawakuwa na dhambi.

Je, haya yote hayaleti wali nyeti ni mtu wa aina gani anayeunganisha sifa hizo zote? Tunamjua mtu ye yote aliyeweza kujisifu kwa kudai sifa mbili tu kati ya hizi kuwa ni zake mwenyewe? Kwenye suala la Yesu, tunaweza kuhitimisha tu kuwa ni mwanadamu asiye wa kawaida. Na hali hiyo ni ya kimungu!

Sasa nigusie kwa kifupi jambo lingine ulilotaja na linaloleta utata hata kwa baadhi ya Wakristo. Ni hili linaloitwa 'utatu' wa Mungu. Hungeweza kugusia mada iliyo ngumu zaida kuitambua. Kuifahamu dhana hii ya kimungu ni sawa na kujaribu kufahamu Mungu ni nani. Acha niseme kinamna kuwa pasipo shaka Wakristo huabudu Mungu mmoja! Tunamwamini Mungu mmoja, kama Biblia yetu inavyofundisha:

> *... Bwana Mungu wako, Bwana ni mmoja.*
> (Kumbukumbu la Torati 6:4)
>
> *"Mimi ndimi Bwana Mungu wako, ... Usiwe na miungu mingine ila mimi."* (Kutoka 20:2, 3)
>
> *Kuna ... Mungu mmoja ambaye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote, katika yote na ndani ya yote.* (Waefeso 4:4-6)

Agano la Kale na Agano Jipya hukubaliana na hili.

Niruhusu niirahisishe mada hii ngumu: Mimi ni mtu mmoja, hata hivyo nina mwili, nafsi na roho. Hivyo mimi ni umoja wa vijenzi vitatu, yaani ni utatu, ingawa unaoonekana ni mwili wangu tu. Mimi si mimi bila ya mwili wangu, nafsi yangu, na roho yangu. Nijaribu, bila kupunguza heshima yake, kuitumia



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 53 13-04-2022 12:22:10

sitiari hii kuhusu nafsi ya Mungu. Biblia humzungumzia Mungu kuwa yeye ni Muumbaji, ni Baba. Hilo halihitaji maelezo mengi.

Lakini pia inamzungumzia Mungu kuwa katika namna ya mwili (Yohana 1:1-5, 9-14; Wafilipi. 2:5-11; Isaya 63:8; Warumi 9:5; Wakolosai 2:9). Huku kulikuwa kwa ajili ya kujifunua mwenyewe kwa wanadamu na kuchukua jukumu la Mwokozi aliyeahidiwa. Huenda kwa kukosa neno lenye ufafanuzi zaidi, Mungu alimtambulisha Yesu kama Mwanawe. Naomba kulizungumzia hilo tena baadaye kidogo.

Tunamjua mtu ye yote aliyeweza kujisifu kwa kudai sifa mbili tu kati ya hizi kuwa ni zake mwenyewe?

Sura au sehemu ya tatu au 'kijenzi' cha tatu ni Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye mngemwita Ru Allah. Kwa Roho wake Mungu huzungumza kwenye mioyo na dhamiri za watu. Kwa Roho wake pia huwaongoza (Yohana 16:7-15). Ili kuepuka miundo migumu ya kitheolojia tuone tu kuwa huyo Mungu mmoja alichagua kujifunua katika maumbo, 'shughuli', au 'nafsi' tatu zilizotajwa. Akijua kutoweza kwetu kulifahamu hili, alichagua kujieleza mwenyewe kwa njia hii, na kwa sababu hiyo inabidi tulikubali hilo. Ingawa inawezekana muundo wangu hautoshi au si kamili, unaonyesha kimsingi dhana ya utatu inahusu nini.

Jina alilotumia Mungu kujifunua mwenyewe katika Biblia ni Yahweh Elohim. Yahweh maana yake ni 'Bwana'. Kiambishi tamati '-im' ya Elohim ya Elohim, huashiria namna ya wingi kwa jinsi ya kiume. Kwa hiyo neno hupaswa kusomeka 'Miungu'. Katika Kumbukumbu 6:4 tunasoma neno alilopewa Musa: "Yahweh (Bwana) Eluhenu (Miungu yetu) Yahweh echad (Bwana ni mmoja, au umoja)."

Muda ulivyoendelea (karne ya 8 kK), Mungu aliielezea 'nafsi' yake kwa ufasaha zaidi kupitia nabii Isaya:



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 54 13-04-2022 12:22:10

> *Nitasimulia juu ya wema wa* B*WANA*, ... *hivyo akawa Mwokozi wao.* [Kiebrania yaani Yesu kwa Kiswahili, kwa maana ya 'Mwokozi'] ... *Lakini waliasi, na kumhuzunisha **Roho Mtakatifu** wake.* (Isaya 63:7-10)

Kwenye Injili Yesu huitwa, **'Mwana wa Mungu'** na **'Mwana wa Adamu'.** Ingawa majina haya huonekana kama yanapingana, ni yule yule. Hili linakuwa wazi kabisa tukiangalia maono aliyopata nabii Danieli:

> *"Katika maono yangu ya usiku nilitazama, na mbele yangu nikamwona anayefanana na* **mwanadamu***, akija pamoja na mawingu ya mbinguni. . . . Akapewa mamlaka, utukufu na ufalme wenye nguvu; nao watu wa kabila zote, mataifa, na watu wa kila lugha wakamwabudu. Utawala wake ni utawala wa milele ambao hautapita, nao ufalme wake ni ule ambao kamwe hautaangamizwa."* (Danieli 7:13, 14)

Tunatambua kuwa hili halimwonyeshi mwanadamu.

Msemo wa 'Mwana wa Mungu' hautaki kuashiria uhusiano wa tendo la ndoa kati ya Mungu na Mariamu, na matokeo yakawa kuzaliwa kwa 'mwanawe'. Lazima tutambue kuwa Mungu ni Roho! Hili hasa huonyesha uhusiano wa kipekee kati ya Yahweh na Yeshua, yaani Mungu Baba na Yesu Mwanawe. Hakuna hata neno moja linalopendekezwa na Biblia katika yale ambayo Waislamu walio wengi hudhani yanafundishwa kwenye Biblia, kuwa Wakristo wanaamini Yesu alikuwa Mwana wa Mungu kimwili. Badala yake Biblia hujua kuwa kwa kila hali hakuna aliye karibu zaidi na baba kuliko mwanawe. Wao ni wa aina moja. Kadhalika na Mungu Baba na Mwanawe Yesu.

Yesu akiwa duniani alizionyesha sifa bainifu zote za kuwa mwanadamu. Alikuwa mtoto aliyekua akiwa na wazazi wake. Alihitaji chakula, kinywaji na usingizi. Inasemekana aliwahi kulia. Hili alilirithi kwa mama yake, kama ninaweza kusema hivyo. Lakini alitembea juu ya maji, alituliza dhoruba na kwa chakula kidogo tu alilisha umati mkubwa ambao kati yao

wanaume walikuwa 5000, wakashiba wote. Aliponya watu wengi mno, alisamehe dhambi, alikuwa na mamlaka kamili juu ya ulimwengu wa mapepo na hata alifufua wafu. Yeye mwenyewe alifufuka katika wafu na akainuliwa hadi mbinguni. Haya yote ni sifa za asili yake ya kimungu. Alifanya yale anayoweza kufanya Mungu peke yake. Hili huonyesha kuwa alikuwa Mwana wa Mungu.

Yesu akiwa duniani, alizionyesha zifa bainifu zote za kuwa mwanadamu.

Matumizi ya jina 'Mwana wa Mungu', kwa kukosa neno lenye ufafanuzi zaidi, yanaweza kuwa ya kimfano kama msemo wa mwana-wa-barabara, ambayo nimeambiwa kuwa ni tafsiri ya neno la Kiarabu kwa maana ya msafiri. Kusudi ni kuonyesha uhusiano.

Biblia hutumia neno la Kigriki 'mono-genis' kumtambulisha zaidi Mwana wa Mungu. Katika Biblia ya zamani ya Kiingereza hilo limetafsiriwa 'only begotten Son', tafsiri inayoweza kutoa wazo kwamba Mungu alimzaa Yesu kimtu. Tafsiri hii haifai na inaweza kupoteza maana halisi ya neno la asili ambayo ni 'mtoto-wa-pekee-wa-aina-yake'. Kwa hiyo Biblia inasema tu kwamba Yesu ana uhusiano wa pekee na Mungu, na hakuna mwingine ye yote mwenye uhusiano wa aina hiyo.

Ninatambua kuwa haya yote yanaweza kuwa mageni sana kwako. Lakini tayari umetambua kuwa Biblia ni ufunuo thabiti kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Tuibishe au hata kuipinga kwa sababu tu tunashindwa kuielewa kikamilifu? La! Sitaki kuhubiri hapa, lakini nikiionyesha tu kweli ya Injili, napenda kukuhimiza ulifikirie hili kwa makini. Kwa sababu mengi ya yale niliyoandika hapa yanapingana na yale uliyofundishwa tangu utotoni, itabidi utumie akili na hoja yako badala ya hisia zako.

Nitasikia kutoka kwako tena! Salamu za upendo!

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 56 13-04-2022 12:22:10

### *Barua ya Kumi*

## Chagua lililo kweli na jema

*Mpendwa Abdallah*

Ninamshukuru Mungu kuwa jibu lako kwa barua yangu ya mwisho, kinyume na hofu ya ndani niliyokuwa nayo, lilinithibitishia kuwa ulikubali uhalali wa kufikiri kimantiki kwenye masuala ya imani, pamoja na utii wako kwa Mungu. Ninaamini kabisa kuwa ni lazima kusimama imara kwa 'miguu' yote miwili kwenye ulimwengu huu wa uongo na udanganyifu. Kielelezo kinaweza kusaidia kuonyesha ninachotaka kusema.

Mguu mmoja uwe kielelezo cha kuwaza kwa utulivu na mantiki.  Lazima tuwe wazi, lakini pia tuwe tayari kujaribu kwa mantiki kila wazo na taarifa (hata yetu wenyewe!) daima tuchunguze kila kinachojitambulisha kama Kweli. Hili hufanikiwa kwa kuchunguza nyaraka, rejea na zaidi ya yote ushahidi unaounga mkono dai kuwa kinatoka kwa Mungu.

Kisha mguu mwingine usimame kama ishara ya kujikabidhi kwa Mungu kwa moyo mmoja usiogawika, ndiyo namna yetu halisi ya ibada, upendo na utii Kwake. Hilo lisifanyike bila ya maombi ya kweli na endelevu kwa Mungu, ili tupate mwongozo sahihi na tuweze kutofautisha kweli na uongo.

Kusimama kwenye 'mguu' mmoja tu hututia kwenye hatari ya kuanguka, kuelemea upande mmoja au kukosa uwiano. Ni rahisi mtu kuwa asiyefundishika, wa kuyumbishwa au anayeshikilia jambo bila ya kutumia akili. Kutulinda na hili Mungu ametupa akili na uwezo wa kuchunguza, kulinganisha na kutoa maamuzi. Hivyo kwanza tulichunguze kwa uaminifu suala la ile kweli, na kisha tujitoe katika utii na ibada kwa Mungu wa pekee wa kweli.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd   57   13-04-2022   12:22:10

Kwa hiyo kwanza tulichunguze kwa uaminifu suala la ile kweli, na kisha tujitoe katika utii na ibada kwa Mungu wa pekee wa kweli.

Hadi sasa nimekutarajia usimame kwa 'mguu' wako wa kuwaza bila upendeleo.Unaweza kuendelea kidogo? Napenda uangalie pamoja na mimi kusulubiwa na kufa kwa Yesu. Mbali na wazo linalobishaniwa la uungu wa Yesu, tuliloangalia kwenye barua iliyopita, msalaba huelekea kuwa mada yenye mhemko zaidi kwenye mazungumzo kati ya Wakristo na Waislamu. Kama nilivyotamka mapema, napenda ukumbuke kuwa kila ninalosema nasema si kwa kusudi la kukuumiza wala kushinda kwenye mabishano. Umuhimu wa sisi kuweza kuangalia pamoja jambo hilo kuhusu kifo cha Yesu na uwezekano wa wewe kutolielewa, unanilemea sana. Hata hivyo naomba tusizizuie mada za 'moto', bali tuzishughulikie kwa upendo.

Wote tunatambua kauli zinazopingana kwenye 'Vitabu' vyetu husika. Kurani hutamka wazi:

> " ... hawakumwua (Isa) wala hawakumsulubu (Wayahudi) ... kwa yakini hawakumwua." (Surah 4:157).

Muktadha hueleza kuwa tukio hili lilionekana tu kwa watu wa wakati huo kana kwamba lilitokea, lakini Mungu alimchukua Isa hadi Kwake. Kinyume chake, kusulubiwa na kufa kwa Yesu kunachukua nafasi kubwa sana kwenye Injili. Hata ni vigumu kutoligundua jambo hili kwenye fundisho la Agano la kale, ambamo huonekana kwa namna ya unabii uliotimia kwenye maisha na kifo cha Yesu.

Ni wazi kuwa haiwezekani mitazamo yote miwili kuwa ni ya kweli. Badala ya kushikamana katakata na misimamo yetu na kubishana ili kutetea tu imani zetu zinazotofautiana, kama inavyotokea mara nyingi, tuutumie tena 'mguu' wetu huo wa



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 58 13-04-2022 12:22:10

kuwaza bila upendeleo. Basi, tuangalie ushahidi wa kuimarisha jibu sahihi.

Kwenye barua ya nyuma tayari nilitaja ushahidi wa unabii uliotimia, habari za mashahidi walioona, taarifa za kihistoria za watu wa wakati ule, na ushahidi wa wachunguzi wa mambo ya kale. Wote Wanavyosema huondoa mashaka yo yote, wote huunga mkono habari ya kusulubiwa na kufa kwa Yesu. Hivyo ni jinsi gani ushahidi huu wote unaweza kupingwa au kubatilishwa kwa dai moja tu lililotamkwa miaka 600 baada ya tukio lililoandikwa, na ambalo halina kabisa ushahidi wa kuunga mkono dai hili?

Kila sadaka ililenga wakati wa mbele,
Yesu atakapokuja kuweka sadaka yake ya
kujitoa mwenyewe mahali pa hizo ishara.

Ninajisikia kutaka kuurudia ushahidi (kama ulivyowasilishwa kwenye barua yangu ya tatu), lakini nitategemea kumbukumbu yako nzuri. Ninajisikia pia kutaka kukushirikisha fundisho la Biblia kuhusu hitaji la sadaka ya kuondoa dhambi, ambayo ni muhimu ya msingi wa kupata msamaha na kupatanishwa na Mungu kama ilivyoandaliwa kwenye enzi ya Agano la Kale. Kila sadaka ililenga wakati wa mbele, Yesu atakapokuja kuweka sadaka yake ya kujitoa mwenyewe mahali pa hizo ishara. Sadaka za mwanzo zilikuwa kivuli tu cha mambo yajayo, tukitumia msemo wa kibiblia.

Yohana Mbatizaji, akimtambua Yesu, alimlenga akisema:

*"Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!"* (Yohana 1:29)

Akiwa bado hai, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuhusu yeye mwenyewe:

*"... Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa viongozi wa makuhani na walimu wa sheria. Nao watamhukumu kifo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 59 13-04-2022 12:22:10

*na kumtia mikononi mwa watu wa Mataifa ili wamdhihaki na kumpiga mijeledi na kumsulubisha msalabani. Naye atafufuliwa siku ya tatu!"*

(Mathayo 20:18-19)

Kisha alisema:

*"... Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi."*

(Mathayo 20:28)

Na hivyo ndivyo ilivyotokea. Nitumie tukio la kihistoria linaloweza kutumika kama mfano.

---

Huenda tukio hili, kuliko lingine lo lote katika historia, huelezea kwa mfano jinsi Yesu alivyoingia kwa ajili yetu ili kuchukua nafasi badala yetu.

---

Shamuel alikuwa mwana mfalme wa Caucasia aliyeishi miaka mamia kadhaa yaliyopita. Watu wake walionekana kuhusika kwenye vita vya kudumu na Waturuki. Siku moja alizingira mji wa Kituruki akitumia jeshi lake. Kama kawaida mama yake alikuwa naye. Usiku mmoja alipanga uvamizi wa kushitukiza, lakini adui alikuwa akisubiri. Mipango yake ya siri ilikuwa imefunuliwa. Akashindwa. Akiwa na huzuni, Shamuel alitangaza kuwa msaliti akikamatwa ataadhibiwa kwa kuchapwa viboko 100. Shambulio lingine likapangwa kwa siri kubwa - lakini matokeo yalikuwa yale yale. Walikuwa wamesalitiwa tena. Lakini wakati huu msaliti alikamatwa. Alikuwa mama wa Shamuel mwenyewe.

Akiwa na maumivu makali moyoni alirudi kwenye hema lake akawa huko siku tatu mchana na usiku. Afanye nini kilicho sahihi? Akimwacha mama yake, wote watakuwa na haki ya kudai kuwa haki imekiukwa kwa kumpenda mama yake. Kwa upande mwingine, akimwadhibu wote watasema: "Tazama mtu yule katili asiye na huruma! Hamhurumii hata



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 60 13-04-2022 12:22:10

mama yake mwenyewe!" Hatimaye Shamuel akajitokeza. Watu wakamzunguka wakitaka kujua. Kisha akawaambia: "Tumeshindwa mara mbili kwa sababu ya usaliti. Tumepoteza watu wengi kwa sababu ya hili. Sioni msaliti ana udhuru wo wote. Kosa lilifanywa, hivyo adhabu itatekelezwa kulingana na sheria yangu kwa viboko 100! Haki na hukumu lazima zidumu!"

Sadaka hii kwa ajili ya dhambi inatosha kwa wanadamu wote nyakati zote, na kwa hiyo haihitaji kamwe kurudiwa.

Mama yake aliletwa katikati akiwa hafifu na kutetemeka kwa hofu. Mtekelezaji wa adhabu akainua kiboko chake - lakini kabla ya mchapo wa kwanza kumjia mama huyu, Shamuel alipiga kelele: "Subiri! Huyu ni mama yangu; mimi ni sehemu ya mwili wake na damu yake. Nitaichukua adhabu badala yake!" Aliingia kwenye mzunguko, akavua vazi lake na kuagiza: "Mtekelezaji wa adhabu, nichape kama ulivyomchapa mhalifu wa mwisho bila ya huruma. Timiza wajibu wako!" Ukaja mchapo baada ya mchapo, hadi Shamuel akazimia. Lakini bila ya kutarajiwa alinusurika kwenye huo msiba uliompata. Tutaweza kujua alivyojisikia mama yake kuhusu alichosababisha kwa mwanawe? Ni lazima mama yake alizidiwa na aibu, mshangao na upendo kwa tabia ya mwanawe.

Huenda tukio hili kuliko tukio lingine lo lote katika historia, huelezea kwa mfano jinsi Yesu alivyoingia kwa ajili yetu ili kuchukua nafasi badala yetu:

> *Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti [msalaba], ili tufe kwa mambo ya dhambi, bali tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa.* (1 Petro 2:24)

Maumivu yake ya kimwili yalikuwa mabaya mno. Hata hivyo hayakuwa maumivu hayo yaliyosababisha mateso ya Yesu, mtu



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 61 13-04-2022 12:22:10

pekee aliye safi bila ya dhambi. Aliteseka kwa kuwa alibeba uchafu wa dhambi *yetu*. Lazima mtu ajisikie kama alivyojisikia mama wa Shamuel.

Haki ya Mungu na upendo wake vilikutana kwenye msalaba wa Yesu.

> *... Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao.* (2 Wakorintho 5:19)

Hili lilitokea mara moja tu. Sadaka hii kwa ajili ya dhambi inatosha kwa ajili ya wanadamu wote nyakati zote na kwa hiyo haihitaji kamwe kurudiwa. Ni neema ya Mungu ikitenda kazi. Ni karama ya Mungu kwetu. Hata hivyo karama huwa yangu tu nikinyosha mkono wangu nikaipokea. Niruhusu nitumie kielelezo kingine:

Mamia machache ya miaka iliyopita, Mwaustria mmoja mchoraji na mpaka rangi alitumwa akatengeneze picha ya kusulubiwa kwa Yesu. Alikuwa ameyaandaa mazingira, akipanga na kupaka rangi michoro yote. Nafasi moja tu nyeupe ilikuwa bado iko wazi kwenye turubai lake. Alikuwa ameitunza kwa ajili ya Mariamu Magdalene, kahaba aliyesamehewa na Yesu akawa mmoja wa wafuasi wake waaminifu. Ila mchoraji na mpaka rangi huyo alimkosa tu mtu sahihi wa kukaa kama mwalikishi mbele yake wakati akichora. Siku moja akiuzungukia Vienna, mji mkuu wa Austria, alishtushwa na mionekano ya mwanamke mhamaji mzururaji (wa kundi la wahamaji wananaodharauliwa wa Ulaya ya Kusini Mashariki). Mchoraji akaona kuwa huyo ndiye "mtu anayekosekana"! Binti huyo alikubali kukaa kwa ajili yake kama 'Mariamu Magdalene', na mchoraji akamchukua hadi kwenye studio ambako mchoro ulisubiri kukamilishwa.

Mwanamke huyo aliutazama mchoro kwa shauku na kusema, "Ni lazima yule mwanaume pale msalabani alikuwa mhalifu mbaya sana kustahili adhabu kama hii." Mchoraji

akasema, “Hapana, ni kinyume chake. Alikuwa mtu mwema sana kabisa!” Yule mwanamke akauliza, “Lakini kwa nini basi watu walimwua?” Huyo mchoraji akaeleza: “Hasa alikufa kwa ajili ya dhambi tulizotenda.” Msichana huyo akauliza baada ya ukimya wenye mawazo, “Kwa ajili ya dhambi zako pia?” Mchoraji akajibu kwa uaminifu, “Ndiyo”. Baada ya kusimama kimya kwenye mawazo msichana huyo akauliza, “Hivyo basi lazima umpende sana sana kabisa.”

Maneno haya yalimgusa, maana hadi wakati huo alikuwa Mkristo wa jina tu. Alizijua habari za Yesu, lakini kamwe yeye binafsi hajawahi kuikubali wala kuitumia maana yenye kina ya ujumbe huu kwenye nafsi yake. Wakati huo utando ulianguka kutoka kwenye macho yake ya kiroho. Alitambua alichofanya Yesu kwa ajili yake yeye binafsi, na alizidiwa na upendo kwa ajili Yake. Kwa hiyo tukio hili likawa mahali pa kugeukia katika maisha yake. Biblia huliita tukio hilo kuokoka, kwa maana ya badiliko - badiliko la moyo.

Itabidi utumie muda kufikiria kwa makini kuhusu ujumbe huu - na kuutafakari moyoni mwako. Unajua kuwa uamuzi wako una viashirio vya milele. Biblia hutuhimiza tufanye uchaguzi sahihi:

> *Leo ninaziita mbingu na nchi kama mashahidi dhidi yako kwamba nimeweka mbele yako uzima na mauti, baraka na laana. Basi sasa chagueni uzima ...* (Kumbukumbu 30:19)

Maswali ya mwisho ni: “Tunajikabidhi kwa nani? Tunasikiliza sauti ya nani? Kuna ushahidi upi kwenye Kweli ambayo Mungu ametoa kwa ajili yetu? Na ushahidi huo kweli unaaminika?”

Ninaomba ubarikiwe kwa kumtambua kikamilifu Mungu na mpango wake na mapenzi yake kwa maisha yako, na uwe na shauku ya kuchagua yaliyo kweli na sahihi!

Wako wa kweli,

*Theofilo*



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 63 13-04-2022 12:22:10

**Rafiki Mpendwa,**

Tunaamini kuwa umefaidika kutoka kwenye barua hizi. Kujibu maswali yafuatayo kutakusaidia kutathmini kwa kina zaidi na kutupa sisi ufahamu wa mawazo yako.

Tutazawadia juhudi zako kwa kijitabu kingine kutoka kwenye machapisho yetu.

1. Ni yapi “mambo yanayokubaliana” ambayo Wakristo na Waislamu hushirikiana?
2. Tupe maoni yako kwenye ombi la mwandishi, “Haitakuwa bora zaidi kukabiliana na masuala kwa uaminifu na kuwa na shauku ya kuipata Kweli?
3. Unaweza kutupa majibu yo yote kwenye maswali “Nani”, “Lini”, na “Wapi” kuhusiana na kupotoshwa kwa Biblia kunakodaiwa?
4. Tutajuaje kama nabii amesema kweli au la? Thibitisha jibu lako kutoka kwenye Maandiko.
5. Kwa nini ni muhimu sana kutambua kuwa kweli na upendo viko pamoja?
6. Jibu letu liwe lipi kwenye ugunduzi wa tofauti za msingi kati ya Uislamu na ufunuo wa Biblia?
7. Ni lipi unaloona kuwa ni tatizo kwenye hoja za Dr. Bucaille kuhusu mafunuo ya kisayansi anayodai kuwa ameyapata kwenye Kurani?
8. Kuna tofauti gani kati ya kauli hizi mbili, “Dhambi ni yale tunayofanya” na “Dhambi ni vile tulivyo”?
9. Elezea kwa maneno yako mwenyewe maana ya “imani” kulingana na Biblia. Kisha ueleze maana yake kwenye Uislamu.
10. Yesu ni nani kulingana na Kurani? Orodhesha sifa zote na maelezo yake.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 64 13-04-2022 12:22:10

11. Kwa nini msalaba wa Yesu huwagawa wanadamu wakawa makundi mawili ya watu?
12. Ni nini hasa maana ya kweli ya "kuokoka"? Umeweza kuokoka, na kama ni hivyo, hilo lina maana gani kwako?

Tafadhali tuma majibu yako pamoja na maswali au maoni mengine yo yote unayoweza kuwa nayo ukitumia anwani yetu.

Asante.



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 65 13-04-2022 12:22:10

**Vijitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya wasomaji wetu:**

1. Umeumbwa kwa Kusudi
2. Jitahidi Kulinganisha
3. Mwisho Usiojulikana
4. Mpendwa Abdallah
5. Mtu Mwenye Ujumbe
6. Kwa nini Kuiamini Biblia
7. Kurani na Biblia
8. Fuata Moyo Wako

Al-Kitab - Kitabu cha Vitabu (kozi ya Biblia kwa njia ya posta)

*Tafadhali nitumie* ........................................................................

..............................................................................................

..............................................................................................

..............................................................................................

Tuma barua yako kwa:

**Hamasa ya Milele**
S.L.P. 11795 Arusha,
TANZANIA
**hymilele@gmail.com**

**Life Challenge**
P.O. Box 50770 - 00200
Nairobi, KENYA
info@life-challenge.org



04-MpendwaAbdallah-Swahili-Edited by SB.indd 66 13-04-2022 12:22:10